# HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2024/2025



MHE. KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB.)
*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*



MHE. *DKT*. DOTO MASHAKA BITEKO (MB.)
*Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati*



**MHE. DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI (MB.)**
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu*
*(Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)*



**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (MB.)**
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu*
*(Sera, Bunge na Uratibu)*



**MHE. PATROBAS PASCHAL KATAMBI (MB.)**
*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu*
*(Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)*



**MHE. UMMY HAMIS NDERIANANGA (MB.)**
*Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu*
*(Sera, Bunge na Uratibu)*



**BI. MARY NGELELA MAGANGA**
*Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu*
*(Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu)*



***DKT*. JIM JAMES YONAZI**
*Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu*
*(Sera, Bunge na Uratibu)*



**BW. ANDERSON MUTATEMBWA**
*Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu*
*(Sera, Bunge na Uratibu)*

# HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM MAJALIWA MAJALIWA (MB.), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KUHUSU MAPITIO NA MWELEKEO WA KAZI ZA SERIKALI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2024/2025

## UTANGULIZI

### Shukrani

*1. **Mheshimiwa Spika***, ninaomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa zilizowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti zilizochambua Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge, Bunge lako sasa lipokee na kujadii Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2023/2024 na Mwelekeo wa Kazi zake kwa Mwaka 2024/2025. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake pamoja na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2024/2025.

*2.* ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa fadhila zake ambazo zimetuwezesha kukutana hapa leo kwa ajili ya kujadili Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Kazi za Serikali kwa Mwaka 2023/2024 na mwelekeo wake kwa mwaka 2024/2025 tukiwa wenye afya njema. Aidha, nitumie fursa hii kuwapongeza Wakristo wote kwa kuhitimisha Kwaresma pamoja na kuadhimisha Sikukuu ya Pasaka kwa mwaka 2024. Vilevile, niwatakie Waislam wote heri ya Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Mwenyezi Mungu atujaalie sote tukamilishe funga zetu.

**Salamu za Pole**

*3.* ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba nitumie fursa hii adhimu kutoa pole kwa Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa *Dkt.* Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania kwa ujumla kwa kumpoteza kiongozi wetu mpendwa Hayati Ali Hassan Mwinyi aliyekuwa Rais wa Awamu ya Pili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, naishukuru Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Mazishi kwa kujitoa kwao usiku na mchana kufanikisha taratibu zote muhimu za maziko sambamba na kuhakikisha kuwa kiongozi wetu anapewa heshima zote za mwisho hadi alipopumzishwa katika Kijiji cha Mangapwani Zanzibar.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** hakika tutaendelea kumuenzi kiongozi huyu mahiri aliyeleta mageuzi ya kisiasa kwa kurejesha mfumo wa demokrasia ya vyama vingi mnamo mwaka 1992, kufungua nchi kiuchumi kwa kuruhusu uwekezaji wa sekta binafsi katika njia kuu za uchumi pamoja na hulka ya ustahamilivu, unyenyekevu na uwajibikaji.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, hivi karibuni tumeondokewa na mwanasiasa nguli na mahiri, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowasa aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nitumie fursa hii kumpa pole Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanafamilia, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa kumpoteza kiongozi huyo ambaye atakumbukwa kwa uthubutu wake, uwezo na ushawishi mkubwa wa kisiasa. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe marehemu pumziko la milele. Amina.

6. ***Mheshimiwa Spika***, tangu tulipohitimisha Mkutano wa 14, nchi yetu imekumbwa na maafa yaliyosababisha athari mbalimbali zikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira. Nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa na mali zao kutokana na maafa hayo. Mwenyezi Mungu awape marehemu pumziko la milele. Amina! Aidha, tunamwomba pia Mwenyezi

Mungu awajalie uponyaji wa haraka ndugu zetu walioumia na ambao bado hawajapona ili waweze kupona na kurejea katika shughuli za ujenzi wa Taifa.

**Salamu za Pongezi**

*7.* ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu tangu ashike madaraka na kuendelea kutuongoza vyema huku tukishuhudia mafanikio lukuki chini ya uongozi wake. Mafanikio hayo yanaonekana dhahiri katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu na huduma za kiuchumi na kijamii ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa vituo vya kutolea huduma za afya, maji, elimu, nishati, uchukuzi na kuimarisha hali ya kisiasa nchini pamoja na mahusiano ya kimataifa.

*8.* ***Mheshimiwa Spika***, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa *Dkt.* Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kuongoza na kusimamia utekelezaji wa mipango ya Serikali yenye kuleta manufaa kwa wananchi na Taifa kwa ujumla. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa *Dkt.* Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake thabiti.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza na kumshukuru Mheshimiwa *Dkt.* Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuendelea kunisaidia katika kuratibu, kufuatilia na kusimamia shughuli mbalimbali za Serikali kwa ufanisi. Hakika, wote mtakubaliana nami kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ameonesha uwezo mkubwa katika utekelezaji wa majukumu aliyopewa na Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee niwapongeze Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, Mbunge wa Chamwino na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; na Mheshimiwa Zainab Athumani Katimba, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI. Ninawatakia kila la heri viongozi wote walioteuliwa katika utekelezaji wa majukumu yao mapya pamoja na kuwakumbusha kuendelea kusimamia kikamilifu mipango ya Serikali na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ili kuhakikisha malengo ya maendeleo tuliyojiwekea yanafikiwa.

*11.* ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabaraza ya Kitaifa Duniani (IPU) na Baraza la Uongozi la IPU ambacho ni chombo kikuu cha kufanya maamuzi kinachojumuisha wabunge kutoka duniani kote. Hakika unastahili pongezi za kipekee kwa kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Bara la Afrika kushika wadhifa huo tangu historia ya kuanzishwa kwa chombo hicho.

*12.* ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, niendelee kukupongeza kwa kuliongoza Bunge hili kwa hekima na umahiri mkubwa. Sina shaka Waheshimiwa Wabunge wenzangu mtakubaliana nami kuwa Mheshimiwa Spika ameendelea kuonesha ukomavu, ustahimilivu na weledi wa hali ya juu katika kusimamia na kuendesha shughuli za Bunge. Hongera sana Mheshimiwa Spika kwa kutekeleza majukumu yako kwa viwango vya hali ya juu.

*13.* ***Mheshimiwa Spika***, nimpongeze pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika pamoja na Mwenyekiti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.) kwa kuendelea kukusaidia kikamilifu kutekeleza majukumu ya kuliongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, kipekee, nimpongeze Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb.), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa ushirikiano alioonesha wakati akihudumu katika nafasi ya Mwenyekiti wa Bunge. Nitoe wito kwetu

sote tuendelee kuwapa ushirikiano ili waendelee kuliongoza vyema Bunge letu na kulifanya liendelee kuheshimika ndani na nje ya mipaka ya nchi yetu.

*14.* ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa *Dkt.* Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria; Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI; Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalumu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti na wajumbe wote wa Kamati hizo kwa michango yao iliyosaidia kuboresha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Mfuko wa Bunge.

*15.* ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ninawashukuru sana Wenyeviti, Makamu Wenyeviti wote pamoja na Wajumbe wa Kamati zote za Kudumu za Bunge lako Tukufu kwa ushauri walioutoa wakati wa kupitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara, Mikoa, Wakala, Idara za Serikali zinazojitegemea na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maoni na ushauri wao utazingatiwa vilivyo wakati wa utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/2025. Aidha, ninamshukuru

Bi. Nenelwa Mwihambi, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano katika utendaji wa majukumu ya kila siku kati ya Serikali na Bunge.

*16.* ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri; Katibu Mkuu Kiongozi; Wakuu wa Mikoa; Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Makatibu Wakuu; Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Naibu Makatibu Wakuu; na Wakuu wa Wilaya, Idara, Mashirika, Wakala na Taasisi zote za Serikali kwa ushirikiano walionipatia na wanaoendelea kunipa wakati wa utekelezaji majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kipekee, niwapongeze na kuwashukuru wafanyakazi wote wa Serikali na taasisi zake kwa kufanya kazi kwa weledi, utaalamu na umahiri mkubwa na hivyo, kuwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

*17.* ***Mheshimiwa Spika****,* kwa namna ya pekee, ninawashukuru Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mbunge wa Peramiho na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); Mheshimiwa Patrobas Paschal Katambi, Mbunge wa Shinyanga Mjini na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) na Mheshimiwa Ummy Hamis Nderiananga, Mbunge wa Viti Maalumu na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Kipekee napenda kumshukuru *Profesa* Joyce Lazaro

Ndalichako (Mbunge), aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) kwa ushirikiano mkubwa aliokuwa akiuonesha wakati wote alipokuwa akitekeleza majukumu yake ndani ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Namtakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yake.

*18.* ***Mheshimiwa Spika***, napenda pia kuwashukuru *Dkt.* Jim James Yonazi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); Bw. Anderson Mutatembwa, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu); Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo; Wakuu wa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu; Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu na wafanyakazi wote kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia. Aidha, nichukue fursa hii pia kumpongeza Bi. Mary Ngelela Maganga kwa uteuzi aliopata na kuwa Katibu Mkuu katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Kipekee nimshukuru *Mhandisi* Cyprian John Luhemeja, Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa ushirikiano mkubwa aliouonesha wakati akitekeleza majukumu yake katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Namtakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yake mapya.

*19.* ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda pia kuwashukuru washirika wa maendeleo zikiwemo taasisi binafsi, nchi rafiki, mashirika ya kimataifa na madhehebu ya dini kwa kuendelea kuunga

mkono juhudi za Serikali za kujenga uchumi shindani wa viwanda na kuiletea nchi yetu maendeleo. Serikali inathamini michango yenu kwenye afua mbalimbali katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2023/2024. Kitendo hicho kimekuwa chachu ya kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.

*20.* ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee na umuhimu mkubwa naomba nitumie fursa hii kuwashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Ruangwa kwa kuendelea kuniunga mkono na kuielewa vizuri dhamana ya Kitaifa niliyonayo ya kusimamia utendaji wa Serikali katika sekta zote na kuwa Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni. Vilevile, niwashukuru Watanzania wote kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Sita ambayo inaendelea kutekeleza kwa dhati dhamira ya kuwaletea maendeleo. Mwisho, kwa umuhimu wa kipekee ninaishukuru familia yangu hususan mke wangu mpendwa, Mary na watoto wetu kwa upendo, dua na kuendelea kunitia moyo ili nitekeleze kwa ufanisi zaidi majukumu niliyopewa ya Kitaifa. Ahsanteni sana.

*21.* ***Mheshimiwa Spika***, huu ni Mkutano wa 15 wa Bunge la 12 ambao ni mahususi kwa ajili ya mjadala wa Bajeti ya Serikali. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tuitumie vyema fursa hii kutoa maoni na ushauri ili kuisaidia Serikali kuimarisha utekelezaji wa vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango na

Bajeti ya Mwaka 2024/2025. Napenda kuwahakikishia kuwa Serikali yenu sikivu ipo tayari kupokea maoni na ushauri wenu na kufanyia kazi kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

*22.* ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya utangulizi huo, ninaomba kuwasilisha makadirio ya bajeti ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa vipaumbele vilivyobainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020; Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/2025, Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050, Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA KIELELEZO KWA MWAKA 2023/2024

*23.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ya kielelezo hususan miradi ya miundombinu ya reli, barabara, viwanja vya ndege, huduma za jamii na nishati yenye mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa letu. Hadi Februari, 2024 utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo:

**Mosi: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Kilomita 1,219)**

Serikali imeendelea kutoa fedha za utekelezaji wa mradi huu ambapo, jumla ya shilingi trilioni 10.69 zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa. Ujenzi wa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (Kilomita 300) umefikia asilimia 98.84, Morogoro – Makutupora (Kilomita 422) umefikia asilimia 96.35, Mwanza - Isaka (Kilomita 341) umefikia asilimia 52.69, Makutupora - Tabora (Kilomita 371) umefikia asilimia 13.86, Tabora - Isaka (Kilomita 165) umefikia asilimia 5.38 na Tabora – Kigoma (Kilomita 506) umefikia asilimia 1.81. Vilevile, hatua za kumpata Mshauri Msimamizi na Mkandarasi wa ujenzi wa reli ya Uvinza – Musongati – Gitega (Kilomita 282) zinaendelea. Kama nyote mlivyoshuhudia, majaribio ya treni hiyo ya mwendo kasi yalifanyika kwa mafanikio makubwa mwezi Februari, 2024. Ni matarajio yetu kuwa huduma ya usafiri na usafirishaji itaanza ifikapo Julai, 2024 kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma. Aidha, reli hiyo ya kisasa itakapoanza kufanya kazi itarahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa baina ya bandari na sehemu za ndani na nje ya nchi.

**Pili:** **Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (Megawati 2,115)**

Mradi wa kuzalisha umeme wa Julius Nyerere ambao utazalisha Megawati 2,115 utekelezaji wake umefikia asilimia 96.81. Kama mlivyoshuhudia zoezi la kuwasha mtambo wa kuzalisha umeme lilifanyika kwa mafanikio na kufanikiwa kuingiza kwenye Gridi ya Taifa Megawati 235. Mtambo huo ni mmoja kati ya mitambo tisa itakayozalisha umeme katika mradi huo. Aidha, kazi zote katika mradi huu zinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Desemba, 2024.

**Tatu:** **Uboreshaji wa Shirika la Ndege Tanzania**

Serikali imekamilisha malipo ya shilingi bilioni 753 kwa ajili ya ndege tatu aina ya Boeing 737-9 Max (ndege mbili) na Boeing 787-8 (ndege moja). Ndege mbili aina ya Boeing 737-9 Max zimewasili nchini Oktoba, 2023 na Machi, 2024 na nyingine moja inategemewa kuwasili Aprili, 2024 na hivyo kulifanya Shirika hilo kuwa na jumla ya ndege 16. Ndege hizo zitawezesha kuongeza safari za ndani na nje ya nchi na kuchochea ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi kama vile utalii, biashara, kilimo, mifugo na uvuvi.

**Nne: Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) lenye urefu wa km 1,443**

Serikali imeendelea kutekeleza Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga. Hadi kufikia Machi, 2024, shughuli zilizofanyika ni pamoja na kukamilisha ulipaji fidia kiasi cha shilingi bilioni 34.93 kwa wananchi 9,823 kati ya 9,904 wanaopisha eneo la mradi; kukamilika na kuzinduliwa kwa kiwanda cha kusimika mifumo ya kupasha joto na kuzuia upotevu wa joto kwenye bomba kilichopo Wilaya ya Nzega; ununuzi na kuwasili kwa shehena nne za mabomba zenye jumla ya kilomita 400; kuanza kwa ujenzi wa matanki manne yenye ujazo wa mapipa 500,000 kila moja ya kuhifadhia mafuta ghafi kabla ya kupakiwa kwenye meli katika eneo la Chongoleani, Tanga; na kuanza kwa ujenzi wa ghati (*jetty*) ya kupakilia mafuta ghafi kwenye meli. Aidha, Serikali kwa ushiriki wake kwenye mradi tayari imechangia jumla ya Dola za Marekani milioni 268.77 sawa na asilimia 87.27 ya hisa zake.

**Tano: Mradi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi**

Serikali imeendelea na ujenzi wa Kiwanda cha Sukari Mkulazi ambapo

ujenzi umefikia asilimia 99 kwa gharama ya shilingi bilioni 320.05. Kiwanda hicho kimeanza uzalishaji Desemba 2023 ambapo hadi kufikia Machi 2024, jumla ya tani 1,851 za sukari zimezalishwa na kupelekwa sokoni. Kuanza kwa uzalishaji kumeongeza kiwango cha upatikanaji wa sukari nchini na kuchangia kuongeza ajira ambapo hadi sasa kiwanda kimetoa fursa za ajira 1,996. Matarajio ya kiwanda ni kuzalisha tani 50,000 kwa mwaka ifikapo mwaka 2026/2027.

**Sita: Mradi wa Daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza)**

Ujenzi wa daraja la Kigongo - Busisi lenye urefu wa kilomita 3.2 pamoja na barabara unganishi yenye urefu wa kilomita 1.66 kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 84.47. Mradi huu utagharimu shilingi bilioni 716.333 ambapo hadi sasa Mkandarasi ameshalipwa jumla ya shilingi bilioni 441.309 na Mhandisi Mshauri ameshalipwa jumla ya shilingi bilioni 6.260. Mradi huu ambao unatarajia kukamilika Desemba, 2024 utasaidia kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii na kuongeza kasi ya maendeleo kwa mikoa ya kanda ya ziwa.

**Saba: Mradi wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, Dodoma**

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato umefikia asilimia 54.1 katika sehemu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya viungio, maegesho ya ndege pamoja na usimikaji wa taa za usalama na kuongozea ndege. Pia, sehemu ya pili inayohusisha ujenzi wa jengo la abiria na majengo mengine utekelezaji umefikia asilimia 17.1. Hadi Februari 2024, jumla ya shilingi bilioni 107.647 zimetumika. Kukamilika kwa ujenzi wa kiwanja hiki kutarahisisha usafirishaji wa watu na bidhaa kutoka na kuingia nchini na hivyo kukuza utalii na uchumi na kuongeza fursa za ajira.

**Nane: Kuboresha Huduma za Usafiri na Usafirishaji kwenye Maziwa Makuu**

Ujenzi wa Meli ya MV. Mwanza "***Hapa Kazi Tu***" umefikia asilimia 93 ambapo Serikali imetumia Dola za Marekani milioni 44.823 sawa na asilimia 90.87 ya gharama zote za mradi huu ambao unatarajiwa kukamilika Mei, 2024. Kukamilika kwa mradi huu kutaboresha huduma za usafiri wa abiria na mizigo kwa njia ya meli katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na nchi za jirani za Kenya na Uganda, na kufungua nchi kiuchumi

pamoja na kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii.

## HALI YA UCHUMI

*24.* ***Mheshimiwa Spika***, uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika licha ya kukumbwa na changamoto kadhaa ambazo baadhi zinatokana na sababu ambazo ziko nje ya uwezo wa Serikali kama vile mabadiliko ya tabianchi, athari za vita na ushindani wa kiuchumi, kisiasa na mikingamo ya kisera ya mataifa makubwa. Katika kipindi cha Januari hadi Septemba 2023, ukuaji wa uchumi wa Taifa ulikuwa asilimia 5.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

*25.* ***Mheshimiwa Spika***, mwenendo mzuri wa ukuaji wa uchumi ni matokeo ya uongozi thabiti wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuchukua hatua mbalimbali za kufungua na kukuza uchumi. Jitihada hizo ni pamoja na kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, kuongeza uwekezaji katika sekta za uzalishaji na huduma za jamii, na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika miradi ya maendeleo.

*26.* ***Mheshimiwa Spika***, kama mnavyokumbuka Mei 2023, Kampuni za *Moody's Investors Service* na *Fitch Ratings* zilikamilisha tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya fedha ya kimataifa. Kwa mujibu wa matokeo ya awali, Tanzania iliwekwa katika daraja la B2 na kampuni ya *Moody's* (*with POSITIVE outlook*) ikimaanisha nchi inaweza kupanda katika nafasi ya juu zaidi huku kampuni ya *Fitch* ikiweka nchi katika daraja la *B POSITIVE* ikiashiria taswira chanya kwa nchi kwenye masoko ya fedha ya kimataifa na uwekezaji.

*27.* ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya mapitio ya uchumi wetu kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita na kujionea mabadiliko makubwa ambayo Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kufanya katika kuboresha uchumi, kampuni ya *Moody's* imechapisha matokeo Machi 2024 ambapo Tanzania imepanda kutoka daraja la chini la B2 (*with Positive Outlook*) na kwenda ngazi ya juu ya B1 (*with STABLE Outlook*). Matokeo hayo ni ya juu kabisa katika ukanda wetu wa Afrika Mashariki na hivyo hatuna budi kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake mahiri uliowezesha Taifa kupata mafanikio hayo.

*28.* ***Mheshimiwa Spika,*** matokeo hayo yana maana kubwa kwa kuwa yanawezesha nchi yetu kuongeza uwezo wa kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (*Foreign Direct Investment*) ambao utaambatana na ongezeko la fedha za

kigeni na ajira. Vilevile, kuongeza wigo wa kukopa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hivyo kuiongezea nchi uwezo wa kutekeleza mipango ya kuwaletea wananchi maendeleo.

*29.* ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka 2024/2025, Serikali imelenga kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa hadi kufikia asilimia 5.4 mwaka 2024 kutoka matarajio ya ukuaji wa asilimia 5.2 mwaka 2023. Ukuaji wa Uchumi utachangiwa na hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa ikiwemo kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa kuwianisha, kufuta au kupunguza viwango vya kodi, tozo na ada zinazoonekana kuwa kero.

**Mfumuko wa bei**

*30.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2023, wastani wa mfumuko wa bei umepungua na kufikia asilimia 3.2 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kiwango hicho kipo ndani ya lengo la nchi la wastani wa asilimia 3.0 hadi 5.0. Kupungua kwa kiwango cha mfumuko wa bei nchini kumechangiwa na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha na bajeti pamoja na upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani.

*31.* ***Mheshimiwa Spika***, mfumuko wa bei nchini unatarajiwa kuendelea kuwa tulivu na kubaki katika wigo wa tarakimu moja wa wastani wa asilimia 3.0 hadi 5.0 na ndani ya vigezo vya

mtangamano wa kiuchumi kikanda kutokana na hatua zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo, kuchochea uzalishaji wa ndani na kupunguza nakisi ya urari wa biashara; usimamizi madhubuti wa sera za fedha na bajeti; utulivu wa thamani ya shilingi na kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini.

**Mwenendo wa Ukusanyaji wa Mapato**

*32.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2023 hadi Januari 2024, mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 17,188.4, sawa na asilimia 95.9 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 17,929.8 na ukuaji wa asilimia 10.0 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2022/2023. Kati ya mapato hayo, mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yalikuwa shilingi bilioni 15,159.8, sawa na asilimia 97.9 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 15,492.7; mapato yaliyokusanywa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali yalikuwa shilingi bilioni 1,374.5, sawa na asilimia 78.2 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 1,758.3; na mapato yaliyokusanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa yalifikia shilingi bilioni 654.1 ikiwa ni asilimia 96.4 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 678.8.

*33.* ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe rai kwa wafanyabiashara wote kuhakikisha wanatoa risiti halali za kielektroniki za mauzo ya bidhaa na

huduma. Vilevile, niwakumbushe wananchi wote kudai risiti halali za kieletroniki kila wanapofanya ununuzi wa bidhaa na huduma, ili kudhibiti upotevu wa mapato na hivyo kuimarisha uwezo wa Serikali kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi ikiwemo maji, elimu na afya.

*34.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Serikali itaendelea kutoa kipaumbele zaidi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi wa bajeti kwa kuendelea kutekeleza hatua zifuatazo: kuimarisha na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na kuwianisha, kufuta au kupunguza viwango vya kodi, tozo na ada zinazoonekana kuwa kero; kuboresha mazingira ya ulipaji kodi na kuongeza wigo wa kodi; kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi; na kuimarisha na kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA ya ukusanyaji wa mapato. Hatua hizi zitawezesha kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kukuza mapato ya ndani hadi kufikia asilimia 15.7 ya Pato la Taifa mwaka 2024/2025 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.3 mwaka 2023/2024.

**UWEKEZAJI**

*35.* ***Mheshimiwa Spika***, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imedhamiria kuifungua nchi katika uchumi wa dunia kupitia utekelezaji wa mikakati

mbalimbali inayolenga kuimarisha mazingira ya uwekezaji hapa nchini. Baadhi ya mikakati iliyotekelezwa ni pamoja na kuboresha miundo ya taasisi za Serikali na kuhamisha baadhi ya majukumu ikiwa ni pamoja na kuhamishia masuala ya uwekezaji katika Ofisi ya Rais kutoka iliyokuwa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Wizara hiyo imeanzishwa mahsusi ili kuimarisha uratibu na usimamizi wa masuala ya uwekezaji.

*36.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha mifumo ya kusajili miradi ili kuongeza idadi ya miradi ya uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Februari 2024, jumla ya miradi 416 ilisajiliwa ambapo miradi ya Watanzania ni 153, wageni ni 175 na ubia ni 88, sawa na ongezeko la asilimia 205 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2022/2023 ambapo jumla ya miradi 203 ilisajiliwa. Miradi hiyo inatarajia kuwekeza jumla ya Dola za Marekani milioni 4,490 na kuzalisha jumla ya ajira 119,717. Uwekezaji huo utaimarisha uchumi wa Taifa pamoja na kuboresha maisha ya watu kupitia fursa za ajira, ukusanyaji wa mapato na kunufaika na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya jamii.

*37.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, kwa kufanya maboresho ya sheria 13 zilizopunguza na kufuta tozo na ada zipatazo 67

kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 ikiwa ni pamoja na kufanya mapitio Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Na. 2 ya 2009, Sheria ya Wakala wa Vipimo Sura ya 340 na Sheria ya Taifa ya Leseni za Viwanda Sura ya 46 kwa kuondoa baadhi ya vipengele ambavyo vilikuwa ni kikwazo katika biashara na uwekezaji nchini.

*38.* ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na jitihada hizo za Serikali, uwekezaji wa sekta binafsi umeongezeka na hivyo kuwezesha uanzishaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo na misitu, kuongeza thamani madini, kutengeneza vifaa vya ujenzi na kuendelea na ujenzi wa kongani za viwanda. Aidha, uwekezaji huu utawezesha matumizi ya malighafi zinazopatikana ndani ya nchi.

*39.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kutunga sera, sheria, kanuni, mikakati na miongozo ili kuweka mazingira wezeshi ya kuvutia uwekezaji nchini; kuhamasisha ushiriki wa Halmashauri na Serikali za Mikoa, sekta binafsi na wadau wa maendeleo katika uendelezaji wa maeneo ya uwekezaji na uendelezaji wa miundombinu ili kuvutia uwekezaji; na kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa wawekezaji katika ngazi zote kwa kuanzisha benki ya ardhi kwa ajili ya uwekezaji na kutenga maeneo kwa ajili ya uwekezaji mahususi.

## UTAWALA WA SHERIA

*40.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya utoaji wa haki na huduma zitolewazo na mahakama kwa kujenga na kukarabati majengo ya mahakama katika ngazi mbalimbali. Hadi Machi, 2024 Serikali imeendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama, Dodoma ambapo ujenzi umefikia asilimia 97 na ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Korogwe, Ulanga na Ubungo unaendelea. Aidha, ujenzi wa mahakama za mwanzo tatu upo katika hatua mbalimbali katika maeneo ya Madale (Dar es Salaam), Kinesi na Rorya katika Mkoa wa Mara.

*41.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji haki kwa kuimarisha mifumo ya kielektroniki ya usikilizaji wa mashauri, utunzaji wa kumbukumbu, ukusanyaji wa takwimu na utoaji wa taarifa za kimahakama unaofahamika kama *Judicial Statistical Dashbord System* pamoja na matumizi ya *Video Conference* katika kuendesha mashauri ya usuluhishi ya kimataifa na hata baadhi ya mashauri ya ndani. Aidha, Mahakama imeanza majaribio ya matumizi ya teknolojia ya akili mnemba ya kunakili na kutafsiri lugha ya mawasiliano wakati wa mwenendo wa usikilizwaji wa mashauri mahakamani. Mifumo hii imewezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake na kuendesha mashauri na utoaji haki kwa haraka.

*42.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuweka taratibu za upatikanaji wa msaada wa kisheria hususan kwa wananchi ambao hawana uwezo wa kumudu gharama za wanasheria. Kwa mwaka 2023/2024, jumla ya wananchi 415,597 walipata msaada wa kisheria ambapo wanaume ni 216,589 wanawake 199,008 kupitia Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia. Aidha, kupitia kampeni hiyo jumla ya migogoro 2,547 iliyohusu ardhi, ndoa, mirathi, matunzo ya watoto ilipokelewa ambapo kati ya hiyo migogoro 223 ilitatuliwa na kuhitimishwa kwa njia ya usuluhishi na upatanishi na migogoro iliyobaki inaendelea kushughulikiwa katika hatua mbalimbali.

*43.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji haki Serikali pia imeendelea kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kutoa huduma za kimahakama pamoja na uandishi wa nyaraka za kisheria. Hadi Januari 2024, umeandaliwa Mwongozo wa Mahakama wa kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika uendeshaji wa kesi na uandishi wa hukumu; sheria kuu 258 na sheria ndogo 15,000 zimetafsiriwa kutoka Kiingereza kwenda Kiswahili.

*44.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Serikali itaendelea kuimarisha utawala wa sheria kwa kuendelea kusimamia mfumo wa haki na utoaji haki; kuimarisha mahusiano na taasisi za kitaifa, kikanda na kimataifa; kuendelea

kuhamasisha matumizi ya njia mbadala za utatuzi wa migogoro ambazo ni usuluhishi, upatanishi, maridhiano na majadiliano ili kurahisisha na kuharakisha upatikanaji wa haki; kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za sheria; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama.

## SEKTA ZA UZALISHAJI

*45.* ***Mheshimiwa Spika***, katika sekta ya kilimo Serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) ya Mwaka 2017/2018 hadi 2027/2028. Katika mwaka 2023/2024, Serikali imefanya mapitio ya kati ya programu hiyo ambapo tathmini ya utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitano ya awali inaonesha ufikiaji wa malengo kwa asilimia 66 ikijumuisha kilimo cha mazao, mifugo na uvuvi. Aidha, pamoja na masuala mengine, matokeo hayo ya awali yanaonesha umuhimu wa kuongeza uwekezaji katika sekta ndogo za mazao na uvuvi ili kufikia malengo.

### Kilimo cha Mazao

*46.* ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuongeza tija na uzalishaji katika mazao kwa kuwezesha wakulima kupata mbegu bora na mbolea, kuwezesha upatikanaji wa zana bora za kisasa za kilimo pamoja na teknolojia za kisasa na rafiki kwa wakulima. Vilevile, kuhakikisha kilimo kinakuwa na faida kwa kuhamasisha uongezaji

wa thamani kwenye mazao na upatikanaji wa masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi. Kutokana na jitihada hizo, katika mwaka 2023/2024, uzalishaji wa mazao ya chakula kitaifa ulikuwa tani milioni 20.4 ikilinganishwa na mahitaji halisi ya tani milioni 16.3. Uzalishaji huo umewezesha nchi kuwa na utoshelevu wa chakula kwa asilimia 124 kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2024/2025.

*47.* ***Mheshimiwa Spika***, sambamba na hilo, Serikali imeendelea kuwekeza katika ujenzi na ukarabati wa skimu za umwagiliaji katika miradi mipya 28 na miradi 30 ya ukarabati yenye jumla ya hekta 95,000 ambayo imefikia wastani wa asilimia 76. Aidha, ujenzi wa mabwawa 11 kati ya 14 umefikia wastani wa asilimia 65. Kukamilika kwa utekelezaji wa miradi hii kutafanya nchi kuwa na hekta 728,223 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji sawa na asilimia 60.69 ya lengo la hekta 1,200,000 ifikapo mwaka 2025.

*48.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo, Serikali imeendelea kutekeleza Programu ya Kuwezesha Ushiriki wa Vijana na Wanawake wenye umri kati ya miaka 18 na 40 katika kilimo biashara ili kujenga kesho iliyobora. Utekelezaji wa programu hii unahusisha miradi minne ya mashamba makubwa ya pamoja, utoaji wa mikopo yenye riba nafuu ya asilimia 4.5 kwa vijana kupitia Mfuko wa Pembejeo wa Taifa, utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima kupitia

vijana wahitimu wa vyuo vya kilimo na uchimbaji wa visima 68,000 kwa ajili ya wakulima wadogo. Hadi Februari 2024, jumla ya ekari 339,092.97 zimebainishwa kwa ajili ya uwekezaji katika Mikoa ya Dodoma, Kigoma, Mbeya, Singida na Kagera.

**Uzalishaji wa Sukari**

*49.* ***Mheshimiwa Spika***, mahitaji ya sukari nchini kwa mwaka 2023/2024 ni wastani wa tani 807,000 ambapo matumizi ya kawaida ni tani 552,000 na mahitaji kwa ajili ya matumizi ya viwandani ni tani 255,000. Katika kipindi hicho uzalishaji wa sukari kwa ajili ya matumizi ya kawaida ulikadiriwa kufikia tani 555,000, wakati uzalishaji halisi ulikuwa tani 367,487.54 sawa na asilimia 66.2 ya lengo. Kutofikiwa kwa lengo la uzalishaji kulitokana na mvua za *El-Nino* kuanzia mwishoni mwa mwaka 2023 ambazo zilileta athari katika uzalishaji kutokana na maji kujaa kwenye mashamba ya miwa na hivyo kuathiri shughuli za uvunaji miwa na kusimama kwa uzalishaji wa sukari katika viwanda vya TPC, Mtibwa, Bagamoyo na Kiwanda cha K1 cha Kampuni ya Sukari Kilombero tangu mwanzoni mwa Novemba 2023.

*50.* ***Mheshimiwa Spika***, hali hiyo ilisababisha upungufu wa sukari na hivyo bei ya bidhaa hiyo kupanda katika maeneo mengi nchini. Ili kukabiliana na uhaba wa sukari uliojitokeza, Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwemo kutoa vibali vya kuagiza tani 100,000 za sukari kutoka nje ya nchi ambapo hadi tarehe 15

Machi, 2024, jumla ya tani 32,085.50 kati ya tani 100,000 zilizoidhinishwa zimeingizwa nchini na usambazaji unaendelea. Pia, kiwanda kipya cha Mkulazi II (Mbigiri) chenye uwezo wa kuzalisha tani 50,000 kilianza uzalishaji Desemba, 2023.

*51.* ***Mheshimiwa Spika***, kwa kuzingatia hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali, napenda kuchukua fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuwa Serikali itachukua hatua zote muhimu kuhakikisha sukari inaongezeka sokoni na kuuzwa kwa bei elekezi. Aidha, hatua za muda mfupi na mrefu zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuratibu uagizaji, usambazaji, kusimamia bei elekezi na kuhimiza wazalishaji kuendelea kuzalisha kabla ya kuanza mvua za masika. Vilevile, kuhamasisha uwekezaji mpya na upanuzi wa viwanda vilivyopo ili kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani 460,048 mwaka 2022/2023 na kufikia tani 706,000 ifikapo mwaka 2025/2026. Aidha, miradi mipya ya Bagamoyo Sugar na Mkulazi II ambayo imeanza uzalishaji inatarajia kuzalisha jumla ya tani 85,000 ifikapo 2025/2026 na hivyo kuwezesha jumla ya uzalishaji kufikia tani 756,000.

**Maendeleo ya Ushirika**

*52.* ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuimarisha ushirika hapa nchini. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha mifumo ya uendeshaji kwa kufanya ukaguzi wa

watendaji wa vyama vya ushirika, kuongeza vitendea kazi, kuongeza usimamizi wa vyama vya ushirika vya kifedha, kutumia mifumo rasmi ya masoko ya mazao ya wakulima, pamoja na kutengeneza Mfumo wa Kidijitali wa Muunganiko wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika. Hadi kufikia Machi 2024, vyama vya ushirika 6,134 kati ya 7,468 vimesajiliwa kwenye mfumo huo. Kutumika kwa mfumo huo kumewezesha kukusanywa tani milioni 1.96 za kahawa na kakao kwa Mkoa wa Mbeya na tani milioni 2.34 za kahawa kwa Mkoa wa Kagera.

*53.* ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali inaendelea kuratibu uanzishwaji wa Benki ya Taifa ya Ushirika kwa kuhamasisha wadau mbalimbali kununua hisa ili kupata mtaji wa shilingi bilioni 20 unaohitajika kuanzisha benki hiyo. Kupitia uhamasishaji uliofanyika, uwekezaji katika hisa umeongezeka kutoka shilingi bilioni 4.7 mwaka 2022/2023 hadi kufikia shilingi bilioni 15.7 Februari, 2024 sawa na ongezeko la asilimia 236. Vyama vya Ushirika vimewekeza jumla ya shilingi bilioni 7.3 sawa na asilimia 72 ya kiasi cha shilingi bilioni 10.2 kilichotengwa kwa ajili ya vyama vya ushirika kuwekeza na kumiliki hisa kwa asilimia 51.

*54.* ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuviwezesha vyama vya ushirika kuwa na nguvu ya pamoja ya soko na kuongeza ushindani wa bei, Serikali imeendelea kuhamasisha wakulima kuuza mazao yao kupitia Mfumo wa Ushirika. Hadi kufikia

Februari 2024, thamani ya mauzo ya mazao ya pamba, korosho, kahawa, tumbaku, ufuta, kakao, mkonge, chai, mbaazi, soya, dengu, miwa na zabibu kupitia mfumo rasmi wa ushirika iliongezeka hadi kufikia shilingi trilioni 1.9 kutoka shilingi trilioni 1.75 mwaka 2022/2023. Vilevile, vyama vya ushirika 147 viliuza kahawa moja kwa moja nje ya nchi kiasi cha tani 13,736 kwa thamani ya Dola za Marekani milioni 40.45.

**Benki ya Maendeleo ya Kilimo**

*55.* ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Februari 2024, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo imetoa mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 160.437 kwa wakulima 159,957 wanaofanya shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi. Vilevile, imetoa dhamana ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 60.80 iliyonufaisha wananchi 10,595 katika shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi kupitia Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo.

*56.* ***Mheshimiwa*** **Spika,** katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kutekeleza Programu ya Kuendeleza Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) pamoja na mapendekezo yatokanayo na mapitio ya programu hiyo ikiwemo uzingativu wa mifumo ya chakula, kuimarisha ushirika, uwezeshaji kwa wakulima ili waweze kuongeza tija katika shughuli za kilimo cha mazao, kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji, kuratibu upatikanaji wa pembejeo, kuboresha huduma za ugani, upatikanaji wa masoko

ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi pamoja na kuimarisha utoshelevu na usalama wa chakula nchini.

**Mifugo**

*57.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kutambua mchango wa sekta ya mifugo kiuchumi na kijamii, imeendelea kuboresha miundombinu ya utoaji wa huduma za mifugo na kuimarisha huduma za ugani. Katika mwaka 2023/2024 Serikali imenunua vifaa tiba 1,100, pikipiki 1,200 na vifaa vya uhimilishaji 184. Vilevile, imeendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa maji kwa mifugo kwa kukamilisha ujenzi wa mabwawa matatu ya Vinyenze (Pwani), Kihumbu (Bunda) na Kongwa (Morogoro DC) pamoja na kuendelea na ujenzi wa mabwawa saba katika Mikoa ya Arusha, Mara, Tanga, Katavi, Manyara, Simiyu na Singida pamoja na utoaji wa mafunzo kuhusu upandaji, uvunaji na uhifadhi wa malisho na mbegu za malisho kupitia mashamba darasa 150 yaliyoanzishwa katika Halmashauri za Wilaya 71.

*58.* ***Mheshimiwa*** **Spika,** Serikali imeendelea kuimarisha ushiriki wa vijana na wanawake katika programu ya BBT ambapo jumla ya vijana 165 wameendelea kupatiwa mafunzo ya kufuga kibiashara ambapo jumla ya ng'ombe 2,176 wamenenepeshwa na kuuzwa kwa thamani ya shilingi bilioni 1.22 na hivyo kupata faida shilingi milioni 153.64. Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za kuanzisha vituo nane (8) vipya vya

BBT katika Mikoa ya Tabora (2), Arusha (2), Morogoro (2), Pwani (1) na Mtwara (1) ili kuwashirikisha vijana wengi zaidi kufuga kibiashara.

*59.* ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya mifugo umeongezeka ambapo uzalishaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita bilioni 3.6 mwaka 2022/2023 hadi lita bilioni 3.9 mwaka 2023/24; usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita milioni 76.9 mwaka 2022/2023 hadi lita milioni 81.8 mwaka 2023/2024; uzalishaji wa zao la nyama umeongezeka kutoka tani 803,264.3 mwaka 2022/2023 hadi tani 838,136.13 mwaka 2023/2024; vipande milioni 14.66 vya ngozi vyenye thamani ya Shilingi bilioni 32.11 vimezalishwa ikilinganishwa na vipande milioni 14.1 vyenye thamani ya Shilingi bilioni 31.1 vilivyozalishwa mwaka 2022/2023; na uzalishaji wa mayai umeongezeka kutoka mayai bilioni 5.5 mwaka 2022/2023 hadi mayai bilioni 5.99 mwaka 2023/2024. Ongezeko hilo limechangiwa na utoaji elimu ya ufugaji bora wa kibiashara na mwitikio wa vijana na wanawake kujishughulisha na ufugaji.

**Uvuvi**

*60.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya sekta ya uvuvi pamoja na kuwapatia wavuvi zana bora, pembejeo na vifaa muhimu vitakavyowawezesha kufanya shughuli zao kwa ufanisi. Katika mwaka 2023/2024, Serikali imeendelea na ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko ambapo ujenzi

umefikia asilimia 42 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 65 kimetumika. Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo Februari, 2025. Vilevile, Serikali imenunua na kusambaza boti 160 za kisasa za uvuvi zenye thamani ya Shilingi bilioni 11.5 kwa vyama vya ushirika wa wavuvi, watu binafsi na vikundi vya wavuvi katika Halmashauri 58. Aidha, Serikali imejenga vizimba 222 katika Mikoa ya Mara, Simiyu, Mwanza, Kagera na Geita kwa ajili ya kuwawezesha wafugaji samaki 1,213 kufanya biashara zao katika mazingira bora.

*61.* ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea na ujenzi wa mabwawa na majosho, kuhamasisha matumizi ya mbegu bora za mifugo na kukamilisha ujenzi wa bandari ya uvuvi, kuendelea na taratibu za ununuzi wa meli za uvuvi wa bahari kuu na kununua boti 520 za kisasa.

**Maliasili na Utalii**

*62.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya sekta ndogo za utalii, wanyamapori, misitu, ufugaji nyuki na malikale na kuhamasisha uwekezaji ili kuhakikisha rasilimali za sekta hizo zinatumika kwa njia endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

*63.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023 tumeshuhudia ongezeko la idadi ya watalii wa Kimataifa kutoka 1,454,920 mwaka 2022 hadi kufikia watalii 1,808,205 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 8.4. Aidha, mapato ya utalii yameongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 2.53 mwaka 2022 hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 3.37 mwaka, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 33.5.

*64.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kutangaza utalii ndani na nje ya nchi ili kuongeza mapato yatokanayo na utalii. Kutokana na mafanikio ya programu ya *Tanzania - The Royal Tour*, Serikali imetengeneza filamu nyingine yenye hadhi ya kimataifa ya kutangaza utalii ya *Amazing Tanzania*. Filamu hii imerekodiwa na Mhe. *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Mhe. *Dkt.* Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mchezaji Filamu nguli kutoka nchini China ajulikanaye kwa jina la Jin Dong. Filamu hiyo imeandaliwa kwa lengo la kuvutia watalii hususan kwa soko la China na inatarajiwa kuzinduliwa Mei, 2024.

*65.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kulinda bioanuai ya hifadhi na kuboresha maisha ya wananchi wanaoishi ndani ya Hifadhi ya Ngorongoro, Serikali imeendelea na zoezi la kuwahamisha kwa hiari wananchi kutoka ndani

ya eneo la hifadhi kwenda katika maeneo yaliyotengwa na Serikali ya Msomera-Handeni, Saunyi-Kilindi, Kitwai-Simanjiro na maeneo mengine ambayo wananchi wamechagua. Katika awamu ya pili, jumla ya nyumba 5,000 zinajengwa katika maeneo ya Msomera (2,500), Saunyi (1,000) na Kitwai (1,500) ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi 21 Februari 2024, jumla ya nyumba 700 zimekamilika na nyumba 1,800 zipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Februari 2024 jumla ya kaya 491 zenye watu 3,451 na mifugo 14,599 wamehama kwa hiari na hivyo kufanya jumla ya kaya zilizohamia tangu kuanza kwa zoezi hili Julai 2022 kufikia 1,042, ikijumuisha jumla ya watu 6,461 na mifugo 29,919.

*66.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Serikali itaendelea kuibua na kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo utalii wa fukwe, meli, mikutano na matukio, michezo na utamaduni; kuimarisha miundombinu katika maeneo ya hifadhi; kuimarisha matumizi na uhifadhi wa maeneo ya malikale kwa kukarabati majenzi ya kale na kuyatangaza; na kuendelea na mikakati ya uongezaji wa thamani ya mazao ya misitu na mazao ya nyuki.

**Madini**

*67.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kusimamia sekta ya madini kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kusimamia masoko

ya madini na vituo vya ununuzi; kudhibiti matukio ya utoroshaji wa madini kwa kuimarisha usimamizi na ukaguzi kwenye maeneo ya uchimbaji, mipakani, viwanja vya ndege na bandarini, kuwezesha na kurasimisha sekta ya wachimbaji wadogo na uwekezaji katika viwanda vya kusafisha dhahabu.

*68.* ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2024 Serikali imeanzisha jumla ya masoko 42 na vituo vya ununuzi wa madini 100 katika maeneo mbalimbali nchini ambapo thamani ya mauzo ya madini katika masoko na vituo vilivyoanzishwa yamefikia shilingi trilioni 1.74 na hivyo kuiwezesha Serikali kunufaika kwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 121.44. Aidha, Serikali imetoa jumla ya vibali 7,775 vya kuuza madini nje ya nchi yenye thamani ya shilingi trilioni 5.82.

*69.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza dhamira yake ya kuweka mazingira wezeshi kwa wachimbaji wadogo wa madini kwa kuwapatia leseni, kuwatengea maeneo maalum na kuwapatia mafunzo yanayohusiana na masuala ya sheria, usalama, afya na utunzaji mazingira. Hadi Februari, 2024 Serikali imetenga jumla ya maeneo 58 yenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,125.92 kwa ajili ya wachimbaji madini wadogo katika mikoa mbalimbali nchini. Leseni 5,586 za uchimbaji mdogo zimetolewa na mafunzo kwa wachimbaji wadogo 9,457 wa Mikoa ya Mara, Simiyu, Mbeya, Geita, Kagera, Mtwara, Lindi na

Dar es Salaam. Vilevile, Serikali ilinunua vifaa mbalimbali vya uchorongaji vyenye thamani ya shilingi bilioni 9.2 kwa ajili ya kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini. Aidha, katika kipindi husika ajira katika migodi na watoa huduma zilifikia 19,165 ambapo ajira 18,580 ni za Watanzania na ajira 585 ni za wageni.

*70.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kusafisha dhahabu kwa kupunguza tozo ya mrabaha kwa madini hususan dhahabu inayopelekwa katika uchenjuaji kutoka asilimia 6 hadi asilimia 4. Lengo ni kuhakikisha viwanda vya kusafisha madini vinapata malighafi ya kutosha katika kipindi chote. Hadi Februari, 2024, Serikali imetoa leseni sita za usafishaji madini ambapo jumla ya dhahabu yenye uzito wa gramu laki 6 na thamani ya shilingi bilioni 84.43 zilipelekwa kusafishwa katika viwanda hivyo.

*71.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Serikali itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa kwa kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya madini ikiwemo madini ya kimkakati; uwekezaji katika kuongeza thamani madini, kufanya tafiti za kina za jiofizikia kwa njia ya kurusha ndege na uendelezaji wa sekta ya wachimbaji wadogo.

## NISHATI

### Umeme

*72.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya upatikanaji wa nishati ya umeme ili kuchochea shughuli za maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kutekeleza miradi mbalimbali. Hadi kufikia Februari 2024, mitambo ya kuzalisha umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ilikuwa na uwezo wa kuzalisha jumla ya Megawati 2,129.85. Hata hivyo, kutokana na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na changamoto za upungufu wa maji katika mabwawa ya kuzalisha umeme iliyokuwepo kabla ya msimu wa mvua za *El-Nino* kuanza, hitilafu kwenye mitambo ya kuzalisha umeme pamoja na upungufu wa gesi asilia katika vituo vya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi, umeme uliozalishwa ulikuwa pungufu kwa Megawati 410.

*73.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma ya umeme nchini katika kipindi cha mwaka 2023/2024, Serikali imekamilisha mradi wa kufua umeme wa Kinyerezi I Extension wenye uwezo wa kuzalisha Megawati 185; mradi wa kuzalisha umeme wa Rusumo ambao umewezesha nchi kupata Megawati 27 na hivi karibuni Serikali imefanikisha kuanza uzalishaji wa umeme kutoka Mradi wa Bwawa la Julius Nyerere kutoka katika mtambo wa kwanza kati ya mitambo tisa ambao unazalisha umeme kiasi cha megawati 235. Miradi mingine inayoendelea

kutekelezwa ni pamoja na miradi ya umeme jua ya Shinyanga megawati 150, Malagarasi Megawati 49.5, na Kakono Megawati 87.

*74.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuongeza miundombinu ya usafirishaji wa umeme kutoka Kilomita 6,111.27 mwaka 2021 hadi Kilomita 7,745.38 Februari, 2024 ili kuwezesha maeneo mengi nchini kuwa na umeme wa uhakika, ambapo mradi wa kusafirisha umeme kutoka *Julius Nyerere Hydro Power Project* hadi Chalinze – kilovoti 400 umekamilika kwa asilimia 99.5; mradi wa kusafirisha umeme wa kilovoti 220 kutoka Geita hadi Nyakanazi umekamilika, mradi wa kusafirisha umeme msongo wa kilovoti 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga umefikia asilimia 99.39, ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme Msongo wa kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Katavi kupitia Sikonge, Ipole na Inyonga umefikia asilimia 55, Mradi wa Kusafirisha umeme kilovoti 220 kutoka Rusumo hadi Nyakanazi na kilovoti 220 kutoka Kinyerezi (Dar es Salaam) hadi Kintinku (Manyoni). Kukamilika kwa miradi hii kutaimarisha njia za kusafirisha umeme nchini na hivyo kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika.

*75.* ***Mheshimiwa Spika***, Serikali katika kutimiza dhamira yake ya kupeleka umeme vijijini, imeendelea na utekelezaji wa miradi ya kusambaza umeme katika vijiji vyote vya Tanzania Bara, ambapo hadi kufikia Februari, 2024 jumla

ya vijiji 11,837 sawa na asilimia 96.1 ya vijiji vyote 12,318 vya Tanzania Bara vimeunganishiwa umeme, ambapo mtandao wa njia za kusambaza umeme nchini umefikia kilomita 176,334.14. Katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kupeleka umeme katika vitongoji; visiwa; vituo vya afya; pampu za maji, machimbo ya madini, viwanda; shule; mahakama za mwanzo vijijini na maeneo yaliyo mbali na Gridi ya Taifa.

**Mafuta na Gesi**

*76.* ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kwa kushirikiana na Kampuni za Nishati za Kimataifa imeendelea na majadiliano kwa lengo la kuendeleza mradi wa uendelezaji wa rasilimali ya gesi asilia iliyogunduliwa katika eneo la bahari kuu kwa ajili ya kuuza nje ya nchi na nyingine kwa ajili ya matumizi ya ndani. majadiliano yanaendelea baina ya Serikali na kampuni za uwekezaji ambapo timu za majadiliano zimekubaliana maeneo mengi na machache yanaendelea kukamilishwa. Timu zitakapokamilisha majadiliano hayo rasimu ya makubaliano itawasilishwa kwa wadau ili kupata maoni kabla ya kusainiwa kwa mkataba hodhi.

*77.* ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea na hatua za utekelezaji wa dhamira ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa mnamo tarehe 01 Novemba, 2022, alipokuwa akifungua mjadala wa Kitaifa wa Nishati Safi ya Kupikia katika Ukumbi wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam

ambapo alielekeza kuandaliwa kwa Mkakati wa Miaka Kumi ya Kuhamia katika Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia kwa asilimia 80 ya matumizi ya nishati ya kupikia nchini.

*78.* ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni hatua ya kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia Barani Afrika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan wakati wa Mkutano wa 28 wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) alizindua Programu ya Nishati Safi ya kupikia itakayowawezesha Wanawake Barani Afrika (*African Women Clean Cooking Support Programme - AWCCSP*) kutumia nishati safi ya kupikia. Katika utekelezaji wa Programu hiyo, mnamo tarehe 9 Februari, 2024 Wizara ya Nishati iliandaa Kongamano la Wanawake la Nishati Safi ya Kupikia Jijini Dodoma ambalo lilifunguliwa na Mheshimiwa *Dkt.* Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kongamano hilo lililenga kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia pamoja na kugawa mitaji na vitendea kazi kwa wajasiriamali wadogowadogo wanawake kutoka mikoa yote Tanzania.

*79.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa maelekezo ya Mheshimiwa Rais, mnamo tarehe 24 Machi, 2023 kupitia notisi namba 1,790, Serikali ilitoa katazo la matumizi ya kuni kwa taasisi za umma na binafsi zinazotoa huduma ya

kulisha watu zaidi ya 100 ziache kutumia kuni na mkaa ifikapo tarehe 31 Januari, 2024 na utekelezaji wa katazo hilo umeanza. Aidha, Serikali imeendelea kuchukua hatua zinazolenga kuhakikisha wananchi wanawezeshwa kutumia nishati safi ya kupikia, ikiwa ni pamoja na kusambaza mitungi ya gesi ya LPG ambapo tayari mitungi 61,400 ya LPG ya kilo 6 imesambazwa kwa wananchi hadi Februari, 2024 kati ya mitungi 70,200 iliyotarajiwa kusambazwa, sawa na asilimia 87. Aidha, usambazaji wa gesi asilia majumbani pamoja na majiko banifu uliendelea.

*80.* ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia nafasi hii kuliarifu Bunge lako kuwa mnamo tarehe 24 Machi, 2024 Serikali imeidhinisha Mkakati wa Miaka Kumi ya Kuhamia katika Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024/2025 hadi 2033/2034. Hatua inayofuata ni utekelezaji wa mkakati huo kwa kuhakikisha wadau wote walioainishwa wanatekeleza majukumu yao katika muda uliopangwa ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

*81.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 pamoja na kumaliza tatizo la mgao wa umeme, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; kupeleka nishati vijijini; kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya mafuta na gesi asilia ikiwa ni pamoja na mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (*Liquefied*

*Natural Gas – LNG Project*) na ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Tanga, Tanzania (*East African Crude Oil Pipeline - EACOP*). Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza shughuli za utafiti na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia; usambazaji wa gesi asilia viwandani, katika taasisi na majumbani na kuimarisha matumizi ya CNG katika magari. Serikali pia itaendelea kuimarisha matumizi ya nishati safi ya kupikia (*clean cooking*) nchini pamoja upatikanaji wa nishati ya mafuta vijijini kupitia uanzishwaji wa vituo vya mafuta katika maeneo hayo pamoja na kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na uhakika wa upatikanaji wa bidhaa za mafuta ya petroli pamoja na ufanisi katika kushughulikia upatikanaji wa bidhaa hizo.

## ARDHI

*82.* ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya ardhi ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi hasa ikizingatiwa kuwa Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na maendeleo ya makazi nchini. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha Ardhi (2018/2019 hadi 2027/2028) imewezesha upimaji wa jumla ya viwanja 46,417 kwenye mikoa 17 nchini ikijumuisha maeneo yaliyo kwenye miradi ya kimkakati. Aidha, programu hii imewezesha kutatua migogoro ya mipaka ya kiutawala ikiwa ni pamoja na mpaka wa Wilaya za Kilindi na Kiteto.

*83.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imefanya utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi kiutawala ambapo jumla ya migogoro 8,700 imetatuliwa kiutawala kupitia Kliniki za Ardhi zinazoendeshwa Mikoa yote Nchini. Azma ya Serikali ni kuhakikisha migogoro ya ardhi inadhibitiwa nchini kwa kupanga, kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi nchini na hivyo kuimarisha usalama wa miliki za ardhi. katika kutekeleza azma hiyo, jumla ya Hatimiliki 92,013, Hati za Hakimilki za Kimila 57,232 na Vyeti vya Vijiji 53 vimetolewa katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Februari, 2024.

*84.* ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa kuboresha makazi, Serikali kupitia Mashirika ya Nyumba imepanga kujenga jumla ya nyumba 7,000 za gharama ya kati na nafuu katika maeneo mbalimbali nchini. Katika utekelezaji wa miradi hiyo mradi wa *Samia Housing Scheme* unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa utajumuisha ujenzi wa nyumba 5,000 katika maeneo mbalimbali. Hadi Machi, 2024 ujenzi wa nyumba 560 kati ya 5,000 unaendelea katika eneo la Kawe Jijini Dar es Salaam.

*85.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kuongeza kasi ya upangaji, upimaji na umilikishaji ardhi nchini; kuendeleza sekta ya makazi; ukamilishaji wa mwongozo wa viwango vya ujenzi wa majengo; na

kukamilisha muswada wa sheria ya ujenzi ambayo itasaidia udhibiti wa ujenzi holela katika miji yetu. Aidha, itaendelea kukamilisha kazi za uthamini kwa wananchi wote wanaopisha shughuli za maendeleo, kuweka alama zinazoonekana ardhini katika mipaka ya vijiji na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji.

**Maendeleo ya Viwanda na Biashara**

*86.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa ustawi wa viwanda na biashara nchini kwa kuandaa na kutekeleza sera, sheria, mikakati na miongozo mbalimbali. Katika mwaka 2023/2024, Serikali imefanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara ya Mwaka 2003 na kuandaa Mkakati wa Taifa wa Utekelezaji Mkataba wa Soko Huru la Afrika. Halikadhalika, Serikali imefanya marekebisho ya Sheria ya Leseni za Biashara na Kanuni zake; Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara; Sheria ya Wakala wa Vipimo; na kufanya maboresho ya mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao ili kurahisisha usajili.

*87.* ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hiyo imeboresha utoaji wa huduma na usimamizi wa shughuli za viwanda na biashara nchini na kuiwezesha Serikali kusajili Makampuni 8,523 kati ya 7,500 yaliyokusudiwa sawa na asilimia 114 na kutoa leseni za viwanda 118 kati ya 100 zilizokuwa zimepangwa sawa na asilimia 118. Vilevile, Serikali imeendelea kuratibu mradi wa

maandalizi ya Kongani ya Viwanda ya Kwala ambapo hadi sasa ujenzi wa barabara kuu ya ndani; jengo la utawala; jengo la zimamoto; jengo la hosteli, majengo mawili ya viwanda na jengo la kufundishia mafundi umekamilika. Aidha, viwanda viwili vimeanza uzalishaji katika eneo hilo.

*88.* ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imeendelea kutumia fursa za masoko yaliyozalishwa kutokana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa ikiwemo Mpango wa Maendeleo ya Biashara kwa Nchi Zinazoendelea (AGOA). Fursa hizi zimechangia kuongeza mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Marekani kupitia mpango wa AGOA kutoka Dola za Marekani milioni 75.1 mwaka 2022 na kufikia Dola za Marekani milioni 80.4 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 7.04. Vilevile, mauzo ya bidhaa kwenda katika soko la Ulaya yaliongezeka na kufikia Dola za Marekani milioni 1,498.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na Dola za Marekani 955.6 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 56.8. Ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za kilimo na viwandani kwenda katika nchi hizo.

*89.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha malengo ya nchi yanafikiwa, Serikali kwa mwaka 2024/2025 itaweka mkazo katika Uendelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya viwanda; uongezaji thamani wa mazao ya kilimo na mifugo kwa kujenga kongani ya viwanda katika mikoa;

urasimishaji wa biashara nchini ili kutoa fursa kwa wafanyabiashara wasio rasmi kunufaika na fursa zilizopo katika soko la ndani, kikanda na kimataifa; na kujenga mifumo ya masoko na utafutaji wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa nchini.

## USAFIRI NA USAFIRISHAJI

*90.* ***Mheshimiwa Spika,*** miundombinu ya usafiri na usafirishaji ni msingi wa uchumi wa Taifa na inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuwezesha na kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Katika kuhakikisha huduma hiyo inaboreshwa, Serikali katika mwaka 2023/2024 iliendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara, viwanja vya ndege, vivuko na majengo ya Serikali.

*91.* ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Februari 2024, Serikali ilikamilisha ujenzi wa kilomita 134.75 za barabara kuu na kilomita 24 za barabara za mikoa kwa kiwango cha lami. Vilevile, imekamilisha ukarabati wa barabara zenye urefu wa kilomita 259.6 kwa kiwango cha changarawe. Pia, Serikali imekamilisha upanuzi wa barabara ya Kimara - Kibaha (kilomita 19.2) kuwa njia nane pamoja na upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji.

*92.* ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa barabara za mijini na vijijini, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na matengenezo ya kawaida ya barabara

zenye urefu wa kilomita 9,838.80, matengenezo ya barabara za lami zenye urefu wa kilomita 115.97, matengenezo ya barabara za changarawe zenye urefu wa kilomita 3,080.87 na ukarabati wa madaraja na makalavati 17 na mifereji ya kuondoa maji barabarani mita 51,309.62.

*93.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya kupunguza msongamano wa magari katika miji na majiji nchini. Jumla ya shilingi bilioni 9.14 fedha za ndani na shilingi bilioni 67.44 fedha za nje zimetumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya mzunguko wa nje wa Jiji la Dodoma yenye urefu wa kilomita 112.3. Hadi kufikia Februari, 2024, ujenzi wa sehemu ya kwanza kutoka Nala - Veyula - Mtumba - Ihumwa Bandari Kavu yenye urefu wa kilomita 52.3 umefikia asilimia 74.17 na sehemu ya pili kutoka Ihumwa Bandari Kavu - Matumbulu - Nala yenye urefu wa kilomita 60 utekelezaji umefikia asilimia 60.62. Ujenzi wa barabara hii unatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba, 2024 na Machi, 2025 kwa sehemu ya kwanza na ya pili mtawalia.

*94.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili Jijini Dar es Salaam unaohusisha *Lot* ya kwanza na ya pili. *Lot* ya kwanza inahusisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 20.3 kutoka Mbagala hadi Mzunguko wa Bandari uliopo eneo la Bendera Tatu; Bendera Tatu hadi Kariakoo; Sokoine hadi

Zanaki; barabara ya Kawawa hadi Magomeni na Barabara ya Chang'ombe hadi Barabara ya Kilwa utekelezaji umefikia asilimia 98. Aidha, kwa upande wa *Lot* ya pili inayohusisha ujenzi wa majengo ikiwemo vituo viwili, yadi moja na vituo mlisho vinne umekamilika. Vilevile, Awamu ya Tatu ya ujenzi wa barabara inayoishia Gongolamboto yenye urefu wa kilomita 23.3 umefikia asilimia 22.2. Kukamilika kwa ujenzi huo kutapunguza msongamano na hatimaye kuchochea ukuaji wa uchumi.

**Viwanja vya Ndege na Usafiri wa Anga**

*95.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na ukarabati, upanuzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege vya Iringa, Musoma, Tabora, Shinyanga, Sumbawanga na Moshi ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya hali ya hewa nchini kwa kukamilisha ufungaji wa rada mbili (2) za hali ya hewa katika Mikoa ya Mbeya na Kigoma, kuendelea na utengenezaji wa rada mbili (2) zitakazofungwa katika Mikoa ya Kilimanjaro na Dodoma ambapo utekelezaji umefikia asilimia 75 na kufunga mitambo mitano (5) ya kutoa huduma za hali ya hewa katika viwanja vya ndege vya Songwe, Zanzibar, Mtwara, Arusha na Songea. Aidha, imekamilisha ununuzi wa mitambo mingine mitatu (3) ya kutoa huduma za hali ya hewa katika viwanja vya ndege vya Musoma, Iringa na Mpanda pamoja na kukamilisha ununuzi wa seti 20 za mitambo ya kupima hali ya

hewa inayojiendesha yenyewe (*Automatic Weather Stations*) katika vituo vya hali ya hewa vilivyopo katika viwanja vya ndege vya Mtwara, Songea na Arusha.

**Reli**

*96.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya reli ya kati kwa kukamilisha ukarabati wa mabehewa ya mizigo 254 na mabehewa ya abiria 25. Vilevile, inaendelea na ukarabati wa kipande cha njia ya reli kutoka Kaliua hadi Mpanda chenye urefu wa kilomita 210 ambacho ukarabati wake umefikia asilimia 10.53.

**Meli**

*97.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya usafiri kwa njia ya maji. Hadi Februari 2024, imekamilisha ukarabati wa meli ya MV Umoja yenye uwezo wa kubeba tani 1,200 ya mizigo kutoka Bandari ya Mwanza kwenda Bandari ya Port Bell nchini Uganda na inaendelea na ukarabati wa MT. Sangara katika Ziwa Tanganyika ambao umefikia asilimia 92. Hatua hii itarahisisha usafiri na usafirishaji wa abiria na bidhaa katika maziwa makuu na nchi jirani ili kuchochea ukuaji wa uchumi. Jumla ya shilingi bilioni 24.13 zimetumika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu hiyo.

**Bandari**

*98.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya bandari nchini kwa kufanya maboresho mbalimbali ikiwemo kuongeza kina cha mita 15.5 na upana wa mita 200 katika lango la kuingia na kugeuza meli kwa ajili ya kupokea meli kubwa katika bandari ya Dar es Salaam. Vilevile, kukamilisha ujenzi wa Gati katika bandari mpya ya Karema Ziwa Tanganyika na kuongeza kina kutoka mita 3 - 13 pamoja na kuboresha Gati Na. 1 - 2 zenye urefu wa mita 450 katika Bandari ya Tanga. Aidha, Serikali imeendelea na ujenzi wa yadi na sakafu ngumu yenye ukubwa wa hekta tano katika Bandari Kavu ya Kwala kwa ajili ya kuhifadhi shehena za mizigo ambapo utekelezaji umefikia asilimia 96 pamoja na kukamilisha ujenzi wa barabara ya zege yenye urefu wa kilomita 15.5 kutoka barabara kuu ya Morogoro hadi Bandari Kavu ya Kwala. Katika kufikia mafanikio hayo, jumla ya Shilingi billioni 69.243 zimetumika.

*99.* ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 2024/2025 Serikali itaendelea kukamilisha miradi inayoendelea ikiwemo ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege, miradi ya kupunguza msongamano katika miji mikubwa, madaraja, uimarishaji wa miundombinu ya reli ya kisasa kwa kiwango cha kimataifa, na uendelezaji wa bandari. Hatua hii itafungua fursa za kijamii na kiuchumi katika maeneo ya utalii, kilimo, mifugo, uvuvi, madini, bandari, viwanda, mafuta na gesi.

## HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

*100.* ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya mawasiliano na teknolojia ya habari nchini kwa lengo la kuongeza chachu ya maendeleo ya jamii, siasa, usalama na uchumi kwa kuzingatia mabadiliko ya sayansi na teknolojia ulimwenguni.

**Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

*101.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali imeendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ambapo hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya kilomita 2,779 za Mkongo zimejengwa pamoja na vituo 111 vya kati vya mawasiliano. Pia, imesambaza mkongo kwenye Wilaya 21 za Rorya, Nachingwea, Ludewa, Newala, Rombo, Same, Mwanga, Hai, Meru, Nanyumbu, Tandahimba, Muheza, Mkinga, Mkuranga, Tunduru, Namtumbo, Mbozi (Vwawa), Ngara, Kyela, Pangani na Muleba. Vilevile, Serikali imeimarisha njia za ndani ya nchi kwa ajili ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa kuunganisha nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, ujenzi wa Mkongo wa Taifa kwenye taasisi 50 katika maeneo ya uwekezaji, vituo vya kutolea huduma ya afya na elimu kwa ajili ya kuwezesha uchumi wa kidijitali unaendelea.

**Uchumi wa Kidijitali**

*102.* ***Mheshimiwa Spika,*** ili kunufaika na fursa zitokanazo na maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani, Serikali imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Kidijitali wa Tanzania (2024 - 2034) unaolenga kuhakikisha nchi yetu inanufaika na fursa za kiuchumi na kujikinga na matishio ya kiulinzi na kiusalama ya mwelekeo wa kidunia wa Mapinduzi ya Nne ya Viwanda yaani *Fourth Industrial Revolution*. Mkakati huu umezingatia mafunzo ya utambulisho kidijitali, ujenzi wa Tanzania kuwa anga la usalama kwa shughuli za mtandao, ukuzaji wa ujuzi wa bunifu za kidijitali, matumizi ya teknolojia zinazoibukia kama vile akili mnemba, ujenzi wa miundombinu ya kisasa ya mawasiliano kama vile satelaiti na mikongo ya baharini. Utekelezaji wa mkakati huu utasaidia kuliandaa taifa letu na wananchi wetu kuweza kuendana na mabadiliko ya kijamii na kiuchumi yatokanayo na Mapinduzi ya Nne ya Viwanda.

**Habari**

*103.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania imeendelea kupanua usikivu wa redio katika maeneo ya mpakani ambapo hadi Februari, 2024 upanuzi wa usikivu umekamilika katika maeneo nane na kuendelea na upanuzi wa usikivu wa TBC katika maeneo 14 na hivyo kuwezesha usikivu wa TBC kufikia asilimia 92 ya nchi na wananchi watapata haki yao ya kikatiba ya kupata habari muda wote.

*104.* ***Mheshimiwa Spika***, katika kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini, Serikali imeendelea kuiwezesha Tanzania Safari Chaneli ambayo imeendelea kuandaa makala zenye ubora wa kimataifa na kurushwa katika majukwaa mbalimbali; kuboresha mpangilio wa vipindi kwa kuzingatia aina ya maudhui; kuandaa makala fupi fupi 50 kwa ajili ya kurushwa ndani ya ndege za ATCL; kuanzisha kipindi kipya cha Safari Tanzania mahsusi kwa ajili ya kuhamasisha utalii na uhifadhi kwa kutumia watu mashuhuri ndani na nje ya nchi ya Tanzania. Kipindi hiki kimeongeza wafuatiliaji wapya 6,500 kwenye mtandao wa *Instagram* kutoka wafuatiliaji 37,400 hadi kufikia wafuatiliaji 43,900 pamoja na kufasiri na kuweka *subtitles* maudhui ya chaneli katika lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kireno, Kiarabu na Kichina ili yaweze kuwafikia watazamaji kutoka ndani na nje ya Tanzania. Maboresho yaliyofanyika yamesaidia kuongeza uelewa wa vivutio vilivyopo nchini na hivyo kuchangia katika ongezeko la watalii kutoka ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

**Anwani za Makazi**

*105.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi kwa kufanya uhakiki wa taarifa za watu na makazi zilizokusanywa wakati wa Operesheni Anwani za Makazi ya Mwaka 2022. Hadi kufikia Februari, 2024, jumla ya anwani milioni 2.24

zimehakikiwa na anwani mpya 498,975 zimesajiliwa katika Halmashauri 25 na kufanya idadi ya anwani zilizohakikiwa na kusajiliwa kufikia milioni 12.84. Vilevile, Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi (NaPA) umeunganishwa na mifumo nane ya taasisi za Serikali ya kutolea huduma ili kuwezesha mifumo hiyo kusomana.

*106.* ***Mheshimiwa Spika***, napenda kusisitiza maelekezo niliyoyatoa hivi karibuni kuzitaka mamlaka za Serikali za Mitaa ziandae sheria ndogondogo kwa ajili ya kulinda matumizi ya vibao vya anwani na kufanya kaguzi za mara kwa mara ya matumizi ya vibao vya anwani ya makazi; kuongeza juhudi katika kupima, kupanga na kutoa namba za nyumba za makazi na ofisi pamoja na kuweka majina ya mitaa katika maeneo mapya; na kuhakikisha vibali vya ujenzi vinatolewa pamoja na taarifa ya anwani za makazi.

*107.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Serikali itatoa kipaumbele katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano, kujenga mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha biashara mtandao, kuimairisha miundombinu ya uchumi wa kidijitali, kuimarisha ulinzi na usalama wa anga ya mtandao na kuimarisha upatikanaji wa habari. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano pamoja utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi ikiwemo ukusanyaji na uhakiki wa taarifa za anwani za makazi.

## HUDUMA ZA JAMII

### Elimu

*108.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa elimu ya msingi na sekondari, hadi Machi, 2024 jumla ya shilingi bilioni 262.62 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa shule za msingi na sekondari, ukarabati wa vyumba vya madarasa, ujenzi na ukamilishaji wa mabweni, mabwalo na uzio wa shule za msingi. Hili limechangia ongezeko la wanafunzi katika mwaka wa masomo 2024 ambapo darasa la awali walioandikishwa ni 1,450,281 sawa na asilimia 77.4 ya lengo, darasa la kwanza ni 1,743,173 sawa na asilimia 92.7 ya lengo na kidato cha kwanza wanafunzi 973,440 sawa na asilimia 89.1 ya wanafunzi waliochaguliwa.

*109.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeongeza fursa za elimu ya juu nchini, ambapo udahili katika vyuo vikuu umeongezeka kufikia wanafunzi 133,617 mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na wanafunzi 113,383 mwaka 2022/2023. Udahili katika Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo umeongezeka kutoka 171,581 mwaka 2022/2023 hadi 235,804 mwaka 2023/2024 na katika Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi udahili umeongezeka kutoka 380,748 mwaka 2022/2023 hadi wanafunzi 415,131 mwaka 2023/2024. Hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na ujenzi wa vyuo 29 vya ufundi stadi, ukarabari wa vyuo 13 vya maendeleo ya wananchi na juhudi za kuendelea na

ujenzi wa miundombinu katika kampasi 14 za vyuo vikuu.

*110.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeongeza fedha za mikopo ya elimu ya juu kutoka shilingi bilioni 654 kwa mwaka 2022/2023 hadi shilingi bilioni 738.7 mwaka 2023/2024. Wanufaika wa mikopo na ruzuku wameongezeka kutoka wanafunzi 177,615 mwaka 2022/2023 hadi wanafunzi 220,278 mwaka 2023/2024. Vilevile, Serikali imeendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi wenye ufaulu uliojipambanua kupitia *Samia Scholarship* ambapo jumla ya shilingi bilioni 9.74 zilitolewa kwa wanafunzi 1,276 wanaoendelea na masomo katika fani za teknolojia, uhandisi, hisabati na tiba.

*111.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali imedhamiria kuinua viwango vya elimu kwa kuongeza fursa na kuboresha mazingira ya upatikanaji wa elimu kwa kila mtoto wa Tanzania. Vilevile, itaendelea kutekeleza mitaala ya elimu na kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya juu pamoja na kuimarisha ufanyaji na matumizi ya tafiti, Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

**Maji**

*112.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji na kujenga mabwawa katika maeneo kame ili

kuongeza uwezo wa nchi kuhifadhi maji ya mvua na kuboresha huduma ya upatikanaji wa majisafi. Lengo la Serikali ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji mijini na vijijini unafikia wastani wa asilimia 95 na 85 mtawalia mwaka 2025.

*113.* ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari 2024, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini imefikia asilimia 79.6 ikilinganishwa na asilimia 77 Februari, 2023. Vilevile, kwa upande wa mijini upatikanaji wa maji umefikia asilimia 90 ikilinganishwa na asilimia 88 Februari 2023. Mafanikio hayo yamechangiwa na kukamilika kwa utekelezaji wa miradi 374 inayonufaisha wananchi wapatao 2,274,193 wanaoishi vijijini pamoja na kukamilika kwa utekelezaji wa miradi 70 ya maji mjini.

**Ujenzi wa Mabwawa**

*114.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilipanga kujenga mabwawa makubwa ya kimkakati ya Kidunda na Farkwa, mabwawa ya kati na mabwawa madogo. Aidha, hadi Februari, 2024 ujenzi wa bwawa la Kidunda linalogharimu shilingi bilioni 329.46 umefikia asilimia 17 na umepangwa kukamilika Juni, 2026. Vilevile, Serikali imeendelea na hatua za maandalizi ya ujenzi wa Bwawa la Farkwa (Dodoma) ambapo wataalam washauri wa kufanya mapitio ya usanifu na usimamizi wamepatikana na wanatarajiwa kukamilisha mapitio Mei, 2024. Kukamilika kwa mabwawa haya kutawezesha maji

kupatikana kipindi chote cha mwaka, kuwezesha kilimo cha umwagiliaji na shughuli za uvuvi.

**Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Maji**

*115.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na utekelezaji wa programu maalum ya Uhifadhi wa Vyanzo vya Maji iliyoanza mwaka 2021 ambapo inatarajia kukamilika mwaka 2035. Kupitia programu hiyo, Serikali imetambua vyanzo vya maji 3,265 vinavyohitaji kuhifadhiwa ambapo vyanzo 316 vimewekewa mipaka na vyanzo 59 vimetangazwa kuwa maeneo lindwa ya vyanzo vya maji.

**Afya**

*116.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya; upatikanaji na usambazaji wa chanjo, dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika ngazi zote. Katika mwaka 2023/2024, Serikali iliendelea kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi, kuimarisha mfumo wa ugharamiaji wa huduma za afya nchini, kuimarisha utoaji wa mafunzo ya wataalam katika Sekta ya Afya, kuimarisha Mifumo ya TEHAMA na matumizi ya takwimu na kuimarisha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika eneo la Afya..

**Bima ya Afya**

*117.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali imetunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2023. Lengo la

kutungwa kwa sheria hiyo ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watanzania wote pindi wanapozihitaji. Aidha, Serikali inaendelea na maandalizi ya Kanuni za Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote zitakazowezesha utekelezaji wa sheria hiyo, ikiwa ni pamoja na kugharamia bima ya afya kwa wananchi wasio na uwezo kwa kuanzisha mfuko maalum wa kugharamia kundi hilo.

**Miundombinu ya Huduma za Afya**

*118.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuweka vifaa kama kompyuta na kamera katika vituo vya afya ili kuwezesha uanzishwaji wa huduma za tiba mtandao (*Telemedicine*). Hadi kufikia Februari 2024, jumla ya hospitali za rufaa 16 na hospitali tatu za rufaa za kanda zimewekewa huduma ya tiba mtandao ambazo ni Iringa, Njombe, Mount Meru (Arusha), Manyara, Singida, Shinyanga, Simiyu, Mwalimu Nyerere Memorial (Musoma), Sekou Toure (Mwanza), Geita, Bukoba, Maweni (Kigoma), Kitete (Tabora), Ligula (Mtwara), Sumbawanga, Bombo (Tanga) Bugando, Benjamini Mkapa na Hospitali ya Kanda – Mbeya.

**Hali ya Upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi**

*119.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi ambapo hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba umefikia wastani wa asilimia 81 katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya ambapo kwa Zahanati imefikia asilimia 77, Vituo vya Afya asilimia 71, Hospitali za Halmashauri asilimia 73, Hospitali za Rufaa za Mikoa asilimia 99 na Hospitali za Rufaa za Kanda, Maalumu na Taifa asilimia 86.

**Mapambano Dhidi ya Magonjwa**

*120.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea na mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza, Serikali kwa kushirikiana na wadau imefanya kampeni na maadhimisho ya kidunia kwa ajili ya kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza kwa kufanya uchunguzi wa mara kwa mara. Kampeni hiyo, iliwezesha kufikia watu 1,107, ambapo takwimu zinaonyesha watu wenye umri wa miaka 30 na kuendelea wana shinikizo la damu la juu, kisukari na uzito uliozidi.

*121.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa, hospitali maalum na hospitali za kanda. Miongoni mwa huduma zilizotolewa ni pamoja na kuweka vifaa vya usikivu kwa watoto 14,

upandikizaji wa figo kwa wagonjwa 12, upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu bila kufungua kifua na mishipa ya damu kwa wagonjwa 413, na wagonjwa wanne kufanyiwa upasuaji wa moyo kwa kupandikizwa mishipa bila kusimamisha moyo kwa mara ya kwanza kwa kutumia wataalam wa ndani. Vilevile, wagonjwa 283 walifanyiwa upasuaji wa goti kwa kutumia matundu, wagonjwa 135 walifanyiwa upasuaji wa ubongo, jumla ya wagonjwa 166 wamewekewa puto tumboni tangu kuanzishwa na wagonjwa 19 wamefanyiwa upandikizaji uloto.

*122.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali imejipanga kuendelea kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi, kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kuanza kwa utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Vilevile, imedhamiria kuimarisha upatikanaji wa huduma bora zinazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi zote pamoja na kuimarisha upatikanaji na udhibiti wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

## HUDUMA KWA MAKUNDI MAALUM

*123.* ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/2024, Serikali imeendelea kutekeleza vipaumbele mbalimbali katika kuimarisha uratibu na uimarishaji wa maendeleo ya jamii, jinsia, wazee,

watoto na makundi maalumu nchini ikiwemo kuimarisha usawa wa jinsia, kuratibu mashirika yasiyo ya kiserikali, kuratibu shughuli za makundi maalum wakiwemo wamachinga, kuendeleza na kuratibu vituo vya kulelea Watoto na Wazee na kuratibu mipango mbalimbali ya kitaifa inayolenga kuendeleza shughuli za maendeleo ya kijamii nchini.

**Usawa wa Jinsia**

*124.* **Mheshimiwa Spika,** Serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Kitaifa ya Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa. Kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 kupitia programu hiyo Serikali imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023, Programu mbalimbali za kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kwa lengo la kuongeza fursa za kiuchumi na kuwajengea uwezo wa mbinu za kibiashara, kupata mitaji, masoko na mikopo. Vilevile, imeanzisha madirisha maalum ya kuwezesha wanawake kupata mikopo yenye riba nafuu ili kupunguza umaskini kwa wanawake kwa kuwawezesha kupata mitaji.

**Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu**

*125.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ambapo mwaka 2023/2024 jumla ya Shilingi bilioni moja ilitolewa kwa ajili ya kuwezesha Mfuko wa Taifa wa Watu wenye Ulemavu. Mfuko huo pamoja masuala mengine utawezesha kutoa

ruzuku kwa Vyama vya Watu Wenye Ulemavu; ununuzi wa vifaa - saidizi; kuwezesha mafunzo ya ufundi stadi na marekebisho kwa Watu Wenye Ulemavu na kufanya tafiti juu ya fursa kwa Watu Wenye Ulemavu. Aidha, Serikali imetumia shilingi milioni 60 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta kinga ya saratani ya ngozi kwa watu wenye ualbino.

*126.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha maisha ya Watu Wenye Ulemavu nchini, mnamo tarehe 02 Desemba, 2023 Serikali ilizindua Mfumo wa Kielektroniki wa Watu Wenye Ulemavu ambao unawezesha kumsajili na kumtambua mtu mmoja mmoja mwenye ulemavu, mahali alipo, shughuli anayoifanya na mahitaji yake. Aidha, kwa kuzingatia kuwa Mfumo huo unaendelea kusambazwa katika Mikoa na Halmashauri zote, nawaelekeza viongozi wote wa mikoa na halmashauri nchini kuhakikisha Mfumo huu unatumika ipasavyo, pamoja na kutenga bajeti ya kuuwezesha kufanya kazi kikamilifu.

*127.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu, kiuchumi, kijamii na kisiasa kwa kuimarisha ushiriki wao katika vyombo vya maamuzi, ushiriki kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, na kuendelea kutoa elimu kwa jamii. Vilevile, Serikali itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Huduma na Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2004, ili kutoa mwelekeo na

mwongozo katika utoaji wa huduma kwa Watu Wenye Ulemavu nchini.

**Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto**

*128.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) kwa lengo la kupinga vitendo vyote vya ukatili kwa wanawake na watoto. Kutokana na utekelezaji wa mpango huo, vitendo vya ukatili kwa wanawake vimepungua nchini kutoka asilimia 40 Mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 22 mwaka 2022. Hii ni kwa mujibu wa Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria 2022.

*129.* ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio haya bado zipo changamoto zinazopelekea kuendelea kwa vitendo vya ukatili ikiwemo kuibuka kwa aina mpya za ukatili kama vile ukatili wa mtandaoni na kuendelea kwa baadhi ya mila na desturi zenye madhara. Ili kuendelea kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeandaa Mpango wa Pili (MTAKUWWA II 2024/2025 - 2028/2029). Mpango huo utaanza kutekelezwa Julai, 2024 na umejumuisha masuala ya uimarishaji wa uchumi wa kaya; mila na desturi; malezi, msaada kwa familia na mahusiano; na mazingira salama shuleni na stadi za maisha.

*130.* ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kukuza usawa wa kijinsia na kutokomeza vitendo vya ukatili, uwezeshaji wanawake kiuchumi, upatikanaji wa haki, ulinzi na malezi chanya ya watoto; kuratibu na kuimarisha utoaji wa huduma za msingi za ustawi wa jamii; kutambua, kuratibu na kuendeleza Makundi Maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo; kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi na Vyuo vya Ustawi na Maendeleo ya Jamii; na kuimarisha ushiriki na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Maendeleo ya Taifa. Aidha, Serikali itatekeleza Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kitaifa wa Kutokomeza Utumikishwaji wa Mtoto 2024/2025 hadi 2028/2029 ambao unajumuisha utekelezaji wa mradi wa kukuza kazi za staha katika kilimo cha pamba katika Wilaya ya Meatu.

**Uratibu wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali**

*131.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kujenga na kuimarisha mahusiano baina ya Serikali, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na wadau wengine kupitia Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Vilevile, Serikali imeandaa na kuzindua ramani ya utambuzi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa njia ya Kidigitali ambayo inasaidia wadau kupata taarifa za Mashirika hayo kwa urahisi ikiwemo mahali ambapo Mashirika yanafanyia kazi, miradi inayotekelezwa, rasilimali zilizopo na wanufaika.

132. ***Mheshimiwa Spika,*** mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa umeendelea kutambuliwa na Serikali ambapo uchambuzi wa mwaka 2022 wa taarifa za mashirika 1,257 ulibaini mashirika hayo yalikuwa na jumla ya mapato ya Shilingi trilioni 2.24 kutoka vyanzo mbalimbali vya fedha. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 1.95 zilitumika kutekeleza miradi 2,412 katika afua za mazingira, afya, uwezeshaji jamii, ulinzi wa jamii, kilimo, elimu, utawala bora, maji, haki za binadamu, nishati, miundombinu na jinsia. Aidha, huduma za mashirika hayo ziliwanufaisha watu 6,316,968 na kutoa ajira 9,818 kwa Watanzania.

## HALI YA SIASA NA DEMOKRASIA NCHINI

133. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 Serikali inayongozwa na Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kutekeleza wajibu wake kwa Watanzania kwa kuzingatia vilivyo misingi ya Maridhiano (Reconciliation), Ustahamilivu (Resilience), Mageuzi (Reform) and Ujenzi mpya (Rebuild). Misingi hiyo ndiyo nguzo kuu ya falsafa ya uongozi wake wenye kulenga kuimarisha misingi ya amani, utawala bora na demokrasia. Misingi hii imekuwa kielelezo cha dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Rais kuona Serikali anayoiongoza inajenga mazingira bora ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Utekelezaji wa falsafa hiyo, ndiyo unaoongoza utekelezaji wa

mipango na mikakati yote ya Serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo shirikishi na endelevu.

*134.* ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha demokrasia nchini inaimarishwa, Bunge lako Tukufu lilitunga Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi na Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria za Vyama vya Siasa. Chimbuko la mapendekezo ya kutunga Sheria Mpya ya Uchaguzi ni kuwepo kwa maudhui yanayofanana ya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 na Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 zinazosimamia uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani. Sheria hizo zinasimamia uchaguzi unaoendeshwa kwa wakati mmoja na kusimamiwa na mamlaka moja ya uchaguzi ambayo ni Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Vilevile, kutungwa kwa Sheria hiyo ni utekelezaji wa maoni ya wadau wa uchaguzi kwamba itungwe sheria itakayoimarisha usimamizi wa uchaguzi nchini.

*135.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kukuza na kuimarisha demokrasia ya vyama vingi nchini, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa imeratibu shughuli za Vyama vya Siasa kwa kuhakikisha fursa sawa zinatolewa katika shughuli za siasa nchini. Katika mwaka 2023/2024, Serikali imetoa ruzuku jumla ya shilingi bilioni 11.7 kwa vyama vya siasa vyenye sifa ya kupata ruzuku. Hatua hii, imesaidia

kuendeleza na kuimarisha uendeshaji wa shughuli za vyama vya siasa na demokrasia nchini. Sambamba na hilo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi imewezeshwa kwa kupatiwa vitendea kazi vipya na shilingi bilioni 77.91 kwa ajili ya maandalizi ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na uendeshaji wa chaguzi ndogo nchini.

*136.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, uchaguzi mdogo wa Ubunge uliendeshwa katika Jimbo la Mbarali na udiwani katika kata 51 Tanzania Bara. Chaguzi hizo zimefanyika kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo vifo na baadhi ya Waheshimiwa Madiwani kukosa sifa za kuendelea na nyadhifa hizo. Nitumie fursa hii kuvipongeza vyama vilivyoonesha ukomavu wa kisiasa kwa kushiriki chaguzi. Kipekee nikipongeze Chama cha Mapinduzi kwa ushindi wa Jimbo la Mbarali pamoja na viti 51 vya udiwani katika chaguzi hizo.

*137.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 yataendelea ikiwa ni pamoja na kuboresha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, kuendelea na utoaji wa elimu ya mpiga kura; kuandaa nyaraka za uchaguzi mkuu na kujenga mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya chaguzi na utoaji wa huduma za Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa.

**Uratibu wa Shughuli za Serikali Bungeni**

*138.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Bunge imeendesha mikutano mitatu ya Bunge yaani Mkutano wa 12, 13 na 14. Katika kipindi hicho, jumla ya maswali ya kawaida 531 na maswali ya nyongeza 1,784 yaliulizwa Bungeni na kujibiwa na Serikali. Aidha, maswali 23 ya papo kwa papo yaliulizwa na kujibiwa na Waziri Mkuu.

*139.* ***Mheshimiwa Spika,*** Bunge lako pia lilijadili na kupitisha miswada 10 ya sheria, maazimio manne ya mikataba na itifaki za Kimataifa. Vilevile, Bunge lilijadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2024/2025. Sambamba na hilo Kamati za Kudumu za Bunge zilifanya uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, Taarifa za Utendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali na ufuatiliaji wa utekelezaji wa afua za UKIMWI.

*140.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Ofisi ya Bunge itaendelea kusimamia shughuli za mikutano minne ya Bunge na mikutano minne ya Kamati za Kudumu za Bunge na kuratibu ushiriki wa Wabunge katika mikutano ya kimataifa ikiwemo Bunge la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, Bunge la Umoja wa Afrika na Mabunge ya Jumuiya ya Madola. Aidha,

Ukumbi wa Bunge utaendelea kuboreshwa pamoja na jengo la kumbi za Bunge na majengo ya ofisi.

**ULINZI NA USALAMA**

*141.* ***Mheshimiwa Spika,*** hali ya ulinzi na usalama katika mipaka ya nchi yetu inayohusisha eneo la nchi kavu, maji na anga imeendelea kuwa shwari bila kuwepo kwa matukio ya uhasama yaliyoripotiwa. Hali hii imechangiwa na ushirikiano uliopo baina ya wananchi na vyombo vya ulinzi na usalama katika kuhakikisha hali ya ulinzi na usalama nchini inaendelea kuimarishwa.

*142.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Jeshi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na Kimataifa katika operesheni za ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Mataifa. Jeshi letu limeendelea kuwa na vikosi vya ulinzi na maafisa wanadhimu na makamanda kwenye operesheni za ulinzi wa amani katika nchi mbalimbali duniani ikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Sudan, Sudan Kusini, Lebanon na Jamhuri ya Afrika ya Kati. Aidha, katika kuimarisha mifumo ya utendaji kazi za ulinzi na usalama wa raia na mali zao nchini, Jeshi la Polisi limeimarisha mifumo ya utendaji kazi kwa kuifikia jamii katika ngazi za mitaa na vijiji kwa kuwapanga Askari Kata katika Kata 3,956 na Shehia 388.

*143.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na usajili na utambuzi wa watu ambapo hadi kufikia Februari, 2024 jumla ya wananchi 24,495,804 wamesajiliwa sawa na asilimia 77.8 ya watu 31,477,938 wenye umri wa miaka 18 na zaidi. Jumla ya namba za utambulisho wa Taifa 20,768,171 zimetolewa kwa wananchi sawa na asilimia 84.8 ya watu wote waliosajiliwa. Vilevile, Serikali imetoa kiasi cha shilingi bilioni 42.5 kwa ajili ya kununua kadighafi 13,514,251 ili kuendelea kuzalisha vitambulisho vya Taifa. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha watu wote wanatambuliwa, kusajiliwa na kupewa vitambulisho.

*144.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali imepanga kufanya usajili wa watoto wote kuanzia umri wa kuzaliwa ili kuhakikisha suala la utoaji wa utambulisho wa Taifa linakuwa jumuishi kwa watu wote. Aidha, Serikali itaanzisha kiwanda cha kuzalisha kadighafi kwa ajili ya matengenezo ya vitambulisho mbalimbali. Hatua hii inalenga kupunguza muda unaotumika kutoa vitambulisho vya Taifa kwa wananchi.

*145.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Serikali itaendelea kuviimarisha vyombo vya ulinzi na usalama kwa kuvipatia zana bora, vitendea kazi vya kisasa, mafunzo pamoja na kuimarisha Mashirika na Taasisi za Utafiti wa masuala ya kijeshi. Vilevile, kuimarisha ushirikiki wa Majeshi yetu kwenye masuala ya ulinzi na

usalama kwenye miamvuli ya Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya za Kikanda na nchi mbalimbali katika nyanja za kijeshi na kiulinzi na kuendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura.

## MASUALA YA KAZI NA WAFANYAKAZI

*146.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi sambamba na kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini, Serikali imeendelea kuimarisha usimamizi wa Sheria za Kazi katika maeneo ya kazi kwa kufanya ukaguzi na kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi.

*147.* ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumshukuru Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza ahadi yake ya ununuzi wa magari 30 aliyoitoa wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani mwaka 2023 Mkoani Morogoro. Magari hayo yamechangia kuimarisha utendaji wa Idara za Kazi za Mikoa pamoja na Wakala wa Usalama Mahali pa Kazi kwa kutoa huduma bora kwa wananchi, wafanyakazi, waajiri na wawekezaji ambapo kaguzi za kazi zimeongezeka kutoka 5,056 mwaka 2022/2023 na kufikia 5,673 Machi 2024. Vilevile, Serikali imeendelea kuboresha mfumo wa majadiliano ya utatu kuhusu masuala ya kazi na ajira miongoni mwa Serikali, Waajiri na Wafanyakazi ili kuweka

fursa na majukwaa ya mashauriano na majadiliano kwa lengo la kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma na uzalishaji katika sekta mbalimbali za uchumi.

*148.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uratibu wa ajira za wageni, Serikali imeendelea kushughulikia maombi ya vibali vya kazi kwa wageni wanaokuja kufanya kazi nchini kwa kuzingatia matakwa ya Sheria, hali inayochangia kwa kiasi kikubwa uwepo wa mazingira rafiki ya ufanyaji kazi, biashara na uwekezaji. Pamoja na kutoa Vibali, uratibu wa ajira za wageni katika kampuni na Taasisi zinazoajiri wageni, umeongeza fursa za ajira kwa wazawa, mfano katika kipindi kinachoishia Desemba, 2023, jumla ya wageni 15,198 na wazawa 318,962 sawa na uwiano wa 1:20 walipata ajira ikilinganishwa na uwiano wa 1:19 ambapo wageni 10,102 na wazawa 192,472 walipata ajira katika kipindi kinachoishia Desemba, 2022 ikiwa ni zaidi ya uwiano wa kisheria wa 1:10. Vilevile, hadi kufikia Machi 2024 makusanyo ya Serikali kupitia vibali vya kazi yamefikia shilingi bilioni 35.33.

*149.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi nchini, kufanya kaguzi katika maeneo ya kazi na kuridhia mikataba ya Shirika la Kazi Duniani ili kuakisi mahitaji ya sasa katika ulimwengu wa kazi,

mazingira ya biashara na kudumisha misingi ya kazi za staha.

### Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kikazi

*150.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, Serikali imeendelea kutatua migogoro ya kikazi kwa njia ya Usuluhishi na Uamuzi. Hadi kufikia Februari, 2024 jumla ya migogoro 2,712 ilitatuliwa kwa usuluhishi na uamuzi kati ya migogoro 4,579 iliyopokelewa. Serikali itaendelea kuongeza kasi ya kutatua migogoro; kusogeza huduma karibu na Wafanyakazi na Waajiri kupitia Tume inayotembea yaani *"Mobile Labour Disputes Settlement Services";* na kuendelea na usimikaji wa mifumo ya kielektroniki ili kurahisisha usajili na utatuzi wa migogoro ya kazi.

### Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri

*151.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 Serikali imeendelea kutoa elimu kwa wadau wa Vyama vya Wafanyakazi, Waajiri na Mashirikisho kuhusu haki ya Uhuru wa Kujumuika ambapo watendaji wa Vyama vya Wafanyakazi 12 kati ya Vyama 33 walipewa elimu na mafunzo kuhusu Haki ya Uhuru wa Kujumuika. Lengo ni kuhakikisha shughuli za uendeshaji wa Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri zinatekelezwa kwa weledi na hivyo kukidhi matarajio ya wanachama wao. Vilevile, Serikali imeendelea kutatua migogoro ndani ya Vyama vya Wafanyakazi kupitia vikao vya majadiliano na

mashauriano ili kubaini changamoto na njia za kutatua changamoto hizo.

*152.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kuratibu na kuhakiki utekelezaji wa majukumu ya Vyama vya Wafanyakazi kwa kufanya kaguzi za utekelezaji wa Sheria na kumbukumbu za kiutendaji; kufanya vikao vya mashauriano na majadiliano kwa Vyama na wadau wengine; kutoa elimu na mafunzo ya kuwajengea uwezo Watendaji wa Vyama kuhusu taratibu na mbinu za uendeshaji wa Vyama. Vilevile, kufuatilia taarifa za wanachama na hesabu za fedha zilizokaguliwa kutoka kwenye Vyama; kupitia na kuchambua Katiba na Kanuni za Vyama vya Wafanyakazi na Waajiri kwa lengo la kumarisha utendaji wa vyama.

**Usalama na Afya Mahali Pa Kazi**

*153.* ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Februari, 2024 Serikali imefanya kaguzi maalum 187,093 sawa na asilimia 66.8 ya lengo la mwaka katika maeneo 13,856. Vilevile, imefanya uchunguzi wa afya kwa wafanyakazi 253,691 ambapo ushauri stahiki ulitolewa. Kutokana na kaguzi hizo Serikali imechukua hatua dhidi ya waajiri 2,360 kwa kutozingatia Sheria na Kanuni za Usalama na Afya Mahali pa Kazi, ambapo kati yao 1,882 walipewa hati ya maboresho, 294 walitozwa faini na 184 walipewa hati ya zuio.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Serikali kupitia OSHA imepanga kufanya kaguzi 300,000 katika maeneo 25,000, kupima afya za wafanyakazi 380,000 na kutoa mafunzo kwa waajiri na wafanyakazi na wajasiriamali wapatao 38,000. Utekelezaji wa mpango huu unalengo la kuendelea kusimamia sheria ya usalama na afya mahali pa kazi ili kujikinga na athari za vihatarishi sehemu za kazi.

**Haki na Uwajibikaji wa Wafanyakazi**

155. ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2022 Serikali ilisanifu Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma wenye Moduli mbili ambazo zinapima utendaji kazi wa mtumishi (PEPMIS) na utendaji kazi wa taasisi (PIPMIS). Mfumo huu unawezesha taasisi na mtumishi kuandaa mipango, kufuatilia utekelezaji, kufanya mapitio, kutathmini utekelezaji na kutoa mrejesho wa utendaji kazi katika kipindi cha mwaka mmoja. Aidha, mfumo unawezesha uchakataji wa mchango wa kila taasisi ya umma katika utekelezaji wa malengo yaliyo katika mipango ya kitaifa. Hadi kufikia Februari 2024, asilimia 88 ya watumishi wa umma wameshajisajili kwenye mfumo huo.

156. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali imepanga kufanya ukaguzi wa kawaida katika taasisi za umma 180 na ukaguzi maalum katika taasisi 10 ili kuhakikisha sheria, kanuni na taratibu za kiutumishi zinazingatiwa.

Mikutano minne ya kisheria ya Tume itafanyika kujadili na kutolea uamuzi rufaa, malalamiko, na masuala mengine ya kiutumishi. Tume pia itahuisha miongozo yake ya uzingatiaji wa masuala ya kiutumishi na kuendelea kutoa elimu kwa wadau katika taasisi za umma na Serikali za mitaa. Aidha, utafiti kuhusu uendeshaji na usimamizi wa rasilimaliwatu katika utumishi wa umma utafanyika.

**Kinga ya Jamii**

*157.* ***Mheshimiwa Spika,*** sekta ya Kinga ya Jamii imekuwa na mchango mkubwa kwenye uchumi pamoja na ustawi wa wananchi kwa ujumla. Sekta ya Kinga ya Jamii imekuwa ikihudumia wananchi wengi ikijumuisha watumishi walio kazini, waliostaafu na kaya maskini. Hadi kufikia Februari, 2024 Sekta hii imekuwa ikihudumia takribani wananchi wasiopungua milioni 16 kupitia Kinga ya jamii ya uchangiaji na isiyo ya uchangiaji.

*158.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) umelipa mafao kwa wastaafu, wategemezi na wanufaika wengine wapatao 29,806 yenye thamani ya shilingi bilioni 927.17 na pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu 168,072 kwa wastani wa shilingi bilioni 70.08 kila mwezi. Aidha, Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umelipa mafao ya Shilingi bilioni 577.7 kwa wastaafu, wategemezi

na wanufaika wengine 89,795. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 79.8 zililipwa kama pensheni ya kila mwezi kwa wastaafu 30,756 ikiwa ni wastani wa shilingi bilioni 9.98 kila mwezi. Vilevile, Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) umelipa mafao ya fidia na pensheni jumla ya shilingi bilioni 12.1 kwa wanufaika wa Mfuko.

*159.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Februari, 2024 Mfuko wa PSSSF umeweza kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 906.46 sawa na asilimia 53.91 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 1,681.56. Vilevile, Mfuko huo umesajili wanachama wapya 29,698 sawa na asilimia 97.55 ya lengo la mwaka la kusajili wanachama wapya 30,444. Usajili huu wa Wanachama kwa kiwango hiki kikubwa umetokana na Serikali kuajiri watumishi wengi mwezi Agosti 2023. Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umekusanya jumla ya kiasi cha ya shilingi bilioni 1,278.15 kutoka kwa waajiri na wanachama wake. Aidha, Mfuko wa WCF umekusanya michango toka kwa Waajiri jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 62.73 sawa na asilimia 67.45 ya lengo la mwaka la kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 93.64.

*160.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) inaendelea na maboresho ya mpango wa Hifadhi ya Jamii kwa wananchi waliojiajiri na wale walio katika sekta isiyo rasmi. Kupitia mpango huu, wananchi

waliojiajiri na wale walio katika sekta isiyo rasmi wanaweza kujiunga na kuchangia kwa hiari kwenye Mfuko, ili kuwawezesha kupata huduma za Hifadhi ya Jamii kama wanavyonufaika wanachama walioajiriwa. Hadi kufikia Februari 2024 jumla ya wanachama 356,741 wameandikishwa kwenye skimu ya uchangaji wa hiari ya sekta isiyo rasmi.

*161.* ***Mheshimiwa Spika,*** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan alielekeza kurejesha michango ya watumishi wote walioondolewa kazini kwa kughushi vyeti. Utekelezaji wa maelekezo hayo ulianza Novemba, 2022 ambapo hadi sasa jumla ya watumishi 14,940 wamerejeshewa michango yao yenye thamani ya shilingi bilioni 45.5 kupitia Mifuko ya PSSSF na NSSF.

*162.* ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kuboresha na kusimamia programu mbalimbali za Kinga ya Jamii nchini ikiwemo kulipa mafao ya wastaafu kwa wakati na kutoa elimu ya mpango wa Kinga ya Jamii kwa wananchi hususan sekta isiyo rasmi. Aidha, Serikali itaimarisha uratibu wa Kinga ya Jamii na kuandaa mkakati wa namna bora ya kugharamia Kinga ya Jamii nchini hususan Kinga ya Jamii isiyo ya uchangiaji *(Social Assistance)* ili kuhakikisha watu wote wanaishi katika viwango vya Kinga ya Jamii vinavyokubalika.

**Ukuzaji wa Fursa za Ajira na Ujuzi**

*163.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu masuala ya uzalishaji wa fursa za ajira nchini kupitia utekelezaji wa miradi ya kielelezo, kujenga mazingira wezeshi kwa wawekezaji na kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi. Katika mwaka 2023/2024, jumla ya fursa za ajira 470,257 zilizalishwa. Kati ya hizo, ajira 248,215 zilizalishwa kupitia Serikali na utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ajira 222,042 kupitia sekta binafsi.

*164.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhakikisha inawezesha nguvu kazi ya Taifa kupata ujuzi wa kuajiriwa na kujiajiri ambapo kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi, Serikali imetoa fursa za mafunzo ya ujuzi kwa vijana 10,702 katika fani mbalimbali kupitia mafunzo ya ufundi stadi kwa njia ya uanagenzi, mafunzo ya ufugaji wa samaki na viumbe maji na mafunzo ya kukuza ujuzi kwa waajiriwa wa Sekta ndogo ya Hoteli na Ukarimu. Serikali imewaunganisha wahitimu 2,448 na mafunzo ya utarajali na mafunzo ya kushindania fursa za ajira kwa wahitimu 7,598.

*165.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na jitihada za kuwaunganisha Watanzania na fursa za ajira nje na ndani ya nchi kwa lengo la kukabiliana na tatizo la uhaba wa ajira nchini. Ili kufikia lengo hili, hadi kufikia Februari,2024 Serikali imesaini Hati tatu za Makubaliano ya

Ushirikiano na nchi mbili za kimkakati ambazo ni Saudi Arabia na Umoja wa Falme za Kiarabu; imeunganisha watanzania 2,019 na fursa za ajira nje ya nchi; na kutoa mafunzo maalumu ya kujenga uwezo kwa watanzania 2,013 wanaokwenda kufanya kazi nje ya nchi.

*166.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Serikali itahuisha Sera ya Ajira ya Mwaka 2008 pamoja na kuweka mazingira bora ya kisheria ya kuratibu uzalishaji wa fursa za ajira na kukuza ujuzi. Aidha, Serikali itaimarisha ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za soko la ajira nchini kupitia mfumo wa kitaifa wa kielektroniki wa taarifa za soko la ajira; kuunganisha Watanzania na fursa za ajira nje ya nchi; kuunganisha wahitimu na mafunzo ya uzoefu kazini; na kutoa mafunzo ya kushindania fursa za ajira nje ya nchi.

## UWEZESHAJI KIUCHUMI

### Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini

*167.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutekeleza Kipindi cha Pili cha Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini katika Awamu ya Tatu ya TASAF katika maeneo yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Mpango huu unaendelea kuwezesha kaya za walengwa kutumia fursa za kuongeza kipato, huduma za jamii na uchumi na kuwekeza katika kuendeleza na kulinda watoto katika kaya hizo.

*168.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024, jumla ya shilingi bilioni 164.31 zimehawilishwa kwa Kaya za Walengwa 1,336,600 katika Halmashauri 184 za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar. Aidha, jumla ya Halmashauri 184 za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar zimeingizwa katika malipo ya njia ya kielektroniki ambayo yanawezesha walengwa kufikiwa kwa haraka na gharama nafuu za uendeshaji.

*169.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea na uhakiki wa kaya za walengwa zilizoimarika kiuchumi katika maeneo yote 186 ya utekelezaji wa mpango. Awamu ya kwanza ya uhakiki ulifanyika kwa walengwa 267,275 ambapo kaya za walengwa zinazokadiriwa kufikia 75,000 zilibainika kuimarika kiuchumi na hivyo kuwa tayari kutoka katika mpango. Awamu ya pili ya uhakiki ulifanyika kwa kaya za walengwa 1,069,325 ambapo uchakataji wa taarifa za kaya hizo unaendelea na utakamilika Aprili, 2024. Aidha, kaya za walengwa zipatazo 1,982 zilizoimarika kiuchumi zilionesha nia ya kujitoa kwa hiari.

*170.* ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya vikundi 56,518 vyenye wanachama 778,940 vya kuweka akiba, kukopeshana na kuwekeza vimeundwa na walengwa katika maeneo ya utekelezaji wa mpango kufikia Machi, 2024. Asilimia 85.1 ya wanachama hao ni wanawake. Vikundi hivyo vimeweza kuweka akiba ya shilingi bilioni 7.9 na kukopeshana shilingi bilioni 3.1. Mpango huo pia

umetoa mafunzo ya stadi za msingi katika shughuli za kiuchumi na kutoa ruzuku ya uzalishaji kiasi cha shilingi bilioni 17.5 kwa kaya za walengwa 51,743 kutoka kwenye maeneo 35 ya utekelezaji.

*171.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo inatarajia kufanya tathmini ya mwisho ya kupima matokeo na manufaa ya mpango huo, ili kuangalia namna ambavyo uwezekezaji wa Serikali umeleta tija katika kuwahudumia wananchi kuweza kuondokana na hali duni na kuboresha maisha yao.

**MAENDELEO YA VIJANA**

*172.* ***Mheshimiwa spika****,* Serikali imeendelea na jitihada za uwezeshaji na uendelezaji vijana kiuchumi ili kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo, kujipatia ajira na kujikwamua kiuchumi. Katika kipindi cha mwaka 2023/2024 kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.27 ilitolewa kwa miradi 56 ya vijana, elimu ya ujasiriamali na usimamizi wa biashara kwa vijana 2,800. Aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya Mwaka 2007 ambayo itawezesha masuala ya vijana kuratibiwa na kutekelezwa na wadau mbalimbali kwa lengo la kuinua ustawi wa vijana nchini.

*173.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kusimamia masuala ya malezi na makuzi kwa vijana nchini; kuandaa mfumo wa kielektroniki wa kusimamia na kuratibu masuala ya maendeleo ya vijana; kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kutoa mikopo ili waweze kujiajiri na kutengeneza fursa za ajira kwa vijana wenzao; kuratibu mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi wa biashara na stadi za maisha kwa makundi maalum ya vijana; kusimamia uundwaji wa vikundi vya vijana vya uzalishaji mali; na kuandaa mfumo thabiti wa uratibu wa shughuli za maendeleo ya vijana nchini.

## MASUALA MTAMBUKA

### Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050

*174.* ***Mheshimiwa Spika,*** ikumbukwe kwamba mnamo tarehe 09 Desemba 2023, Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alizindua rasmi mchakato wa maandalizi ya Dira mpya ya Maendeleo ya Taifa. Dira hiyo itatoa mwongozo wa mwelekeo wa maendeleo ya nchi kwa kipindi cha miaka zaidi ya 25 ijayo.

*175.* ***Mheshimiwa Spika,*** niendelee kutoa rai kwenu Waheshimiwa Wabunge na kwa Watanzania wote kushiriki kikamilifu katika zoezi la kutoa maoni ambayo yatatuwezesha kuwa na Dira mpya ya Taifa ya Maendeleo itakayobeba

maono ya muda mrefu na kujumuisha masuala yote muhimu kwa ajili ya kuwa na maendeleo endelevu yenye kuzingatia ustawi wa jamii ya kitanzania.

**Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024**

*176.* ***Mheshimiwa Spika,*** sote tunafahamu kuwa mwaka 2024 kutakuwa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Serikali inaendelea na maandalizi ya uchaguzi huo ambapo hadi Februari, 2024 imetoa shilingi bilioni 5.1 kwa ajili ya maandalizi ya uchaguzi huo ikiwemo uhakiki wa maeneo ya uchaguzi, kuandaa Tangazo la Serikali, kuandaa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa pamoja na kuhakiki vituo na vifaa vya uchaguzi.

*177.* ***Mheshimiwa Spika***, Serikali itahakikisha uchaguzi huo unafanyika kwa kuzingatia sheria, kanuni na misingi ya kidemokrasia. Aidha, nitoe wito kwa wadau wote wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa kushiriki kikamilifu katika mchakato wote wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kuwezesha uchaguzi huo kuwa wa mafanikio.

**Mapambano Dhidi ya Rushwa**

*178.* ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kupambana na kudhibiti vitendo vya rushwa na ufisadi nchini ambapo hadi kufikia Februari, 2024 kesi 767 zimeendeshwa katika mahakama mbalimbali. Kati ya kesi hizo, kesi 254 ziliamuliwa mahakamani ambapo Jamhuri ilishinda kesi 169 na

watuhumiwa kuhukumiwa kifungo na kulipa faini. Aidha, shilingi bilioni 14.45 ziliokolewa kutokana na operesheni za uchunguzi zilizofanyika katika maeneo mbalimbali nchini ambapo shilingi bilioni 13.79 ni fedha taslimu zilizorejeshwa Serikalini na shilingi milioni 789.78 zilidhibitiwa.

*179.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TAKUKURU imefuatilia miradi ya maendeleo 891 yenye thamani ya shilingi bilioni 644.06 kwa ajili ya kubaini viashiria vinavyoweza kusababisha upotevu wa rasilimali za umma na thamani ya fedha isifikiwe. Katika ufuatiliaji huo, miradi 160 yenye thamani ya shilingi bilioni 54.01 ilibainika kuwa na kasoro mbalimbali na inaendelea kufanyiwa uchunguzi ili hatua stahiki zichukuliwe.

*180.* ***Mheshimiwa Spika***, juhudi za kupambana na rushwa zimeiletea sifa nzuri nchi yetu kikanda na kimataifa. Kwa mujibu wa Taarifa ya *"Transparency International"* ya mwaka 2023, Tanzania kwa kupitia kiashiria cha kipimo cha mtazamo wa rushwa katika jamii *"Corruption Perception Index"* imeendelea kufanya vizuri kwa kupata alama 40 na kushika nafasi ya 87 kati ya nchi 180 ikilinganishwa na alama 38 na nafasi ya 94 iliyopata mwaka 2022. Kwa matokeo haya Tanzania imepanda kwa nafasi saba.

*181.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Serikali itaendeleza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi kwa kuelimisha umma kuhusu madhara ya rushwa, kuchambua na kuimarisha mifumo ya utendaji kazi na utoaji huduma, kuchunguza na kuwafikisha mahakamani watuhumiwa wa rushwa na ufisadi, na kuendelea kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ili kuongeza ufanisi kwenye kukabiliana na rushwa hapa nchini.

**Mapambano Dhidi ya UKIMWI**

*182.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu na kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI nchini. Katika mwaka 2023/2024 Serikali imezindua taarifa ya Matokeo ya Utafiti wa Athari za UKIMWI Tanzania wa mwaka 2022/2023. Utafiti huu umeonesha matokeo chanya yaliyofikiwa na nchi yetu katika mwitikio dhidi ya UKIMWI ikiwemo kupungua kwa kiwango cha ushamiri wa VVU kutoka asilimia 4.7 mwaka 2016/17 hadi asilimia 4.4 mwaka 2022/2023 pamoja na kupungua kwa maambukizi mapya kutoka watu 87,013 mwaka 2016/2017 hadi watu 60,000 mwaka 2022/2023.

*183.* ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu ipo kwenye mwelekeo mzuri wa kufikia shabaha za kitaifa na kimataifa za 95-95-95 ifikapo 2026. Utafiti huo umebainisha kuwa asilimia 95 ya kwanza inayohusu watu wote wanaoishi na VVU kupima na kujua hali zao za maambukizi imefikia

asilimia 82, asilimia 95 ya pili inayohusu Tiba kwa WAVIU waliotambua hali zao imefikia asilimia 97 na asilimilia 95 ya Tatu inayohusu Ufubazaji wa Virusi kwa WAVIU wanaoendelea tiba imefikia asilimia 94.

*184.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Serikali itaendeleza jitihada za mapambano dhidi ya UKIMWI kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo kutoa fedha za mitaji kwa Wasichana Balehe na Wanawake Vijana; kutekeleza programu za kuhamasisha upimaji wa hiari; kufanya Mapitio ya Sera Taifa ya Kudhibiti UKIMWI ya Mwaka 2001; kuwezesha shughuli za uendeshaji wa Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI; kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa afua za VVU na UKIMWI; na kutoa elimu kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi ya kupata VVU na kujenga uwezo kwa viongozi wa kisiasa, dini, kimila na mitandao ya makundi maalumu yaliyo katika mazingira ya hatari zaidi ya kupata maambukizi ili kushughulikia mila na desturi zinazosababisha unyanyapaa na ubaguzi wa kijinsia.

**Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya**

*185.* ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imepata mafanikio makubwa katika udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya ambapo hadi kufikia Desemba 2023, jumla ya kilogramu milioni 1.96 za dawa za kulevya zilikamatwa kutoka kwa watuhumiwa 10,522. Aidha, dawa tiba zenye asili

ya kulevya kilogramu 1.95 na lita 61.67 zilikamatwa. Kiasi hicho kilichokamatwa ni zaidi ya jumla ya dawa za kulevya zilizokamatwa nchini katika kipindi cha miaka 11 kuanzia mwaka 2012 hadi 2022 ambazo ni kilogramu 660,465.4. Mafanikio haya yameipa heshima nchi yetu kimataifa kwa kupewa tuzo mbalimbali kutokana na udhibiti uliooonesha ufanisi mkubwa ndani na nje ya mipaka ya nchi.

*186.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ilifanikiwa kuteketeza ekari 2,389 za mashamba ya bangi katika mikoa ya Arusha ekari 1,093, Morogoro ekari 489, Mara ekari 807 na ekari 535 za mashamba ya mirungi katika Mkoa wa Kilimanjaro. Vilevile, ulifanyika ukaguzi kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa biashara ya kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya. Ukaguzi huo ulifanyika katika maeneo mbalimbali 734 katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Mwanza, Songwe, Shinyanga, Dodoma na Kilimanjaro. Halikadhalika, kupitia mifumo ya kielektroniki, Serikali ilifanikiwa kuzuia kemikali bashirifu kilogramu 157,738.55 na lita 1,000 zilizokuwa ziingizwe kinyume cha sheria ambazo kama zingechepushwa zingeweza kutumika kutengenezea dawa za kulevya. Pia, juhudi hizi zimekwenda sambamba na uzinduzi wa Mwongozo wa Uelimishaji Kuhusu Rushwa na Dawa za Kulevya utakaotumika kwenye Klabu za Kupinga Rushwa na Dawa za Kulevya Shuleni na Vyuoni; kukamilisha Sera ya Kudhibiti na Kupambana na

Dawa za Kulevya ya Mwaka 2023 na kuanzisha maabara ya uchunguzi na sayansi jinai.

*187.* ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/25 Serikali itaendeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kutekeleza afua za kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya nchini; kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya; kupunguza madhara yanayosababishwa na utumiaji wa dawa za kulevya; na kuboresha ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa.

**Uratibu wa Maafa**

*188.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhakikisha shughuli za kuzuia na kupunguza madhara ya majanga na kujiandaa kwa ajili ya maafa yanayoweza kutokea zinatekelezwa kikamilifu. Kufuatia taarifa ya tahadhari iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kuhusu kutokea kwa mvua za El-Nino, Serikali iliandaa Mpango wa Taifa wa Dharura wa Kukabiliana na Madhara ya El-Nino kwa kipindi cha Septemba, 2023 mpaka Juni, 2024. Kupitia mpango huo, Kamati za Usimamizi wa Maafa za Mikoa 18 na timu za utayari zilijengewa uwezo katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Januari, 2024 zikijumuisha Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Tanga, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Shinyanga, Simiyu, Mwanza, Mara, Geita, Kagera, Kigoma, Lindi, Mtwara, Ruvuma na Tanga.

*189.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendelea kuratibu na kutoa huduma za kibinadamu wakati wa maafa ikiwemo makazi ya muda, chakula, vifaa vya ujenzi, vifaa vya malazi, vifaa vya usafi, matibabu na huduma za kisaikolojia katika maeneo mbalimbali yaliyokumbwa na maafa hapa nchini. Katika mwaka 2023/2024 ufuatiliaji wa hali ya majanga na uratibu wa misaada ya kibinadamu umefanyika katika Wilaya za Ilala, Kinondoni, Temeke, Kigamboni, Ubungo, Kilosa, Same, Moshi, Hai, Muleba, Bukoba, Mbarali, Nyang'wale, Mbogwe, Chato, Ruangwa, Shinyanga, Hanang, Masasi, Mbarali, Newala, Kakonko na Liwale. Vilevile, Serikali imekamilisha ujenzi wa maghala mawili ya kuhifadhi vifaa vya misaada ya kibinadamu na kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa Dodoma ambapo ujenzi umefikia asilimia 37.

*190.* ***Mheshimiwa Spika,*** sote tumeshuhudia uratibu madhubuti wa Serikali katika maafa yaliyotokea tarehe 03 Desemba, 2023 wilayani Hanang, Mkoa wa Manyara kufuatia maporomoko ya udongo ulioambatana na mawe, miti, magogo na tope. Maafa hayo yalisababisha madhara mbalimbali ikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa miundombinu, makazi na mazingira. Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na kurejesha hali ikiwemo kufanya uokoaji, kuanzisha kambi za muda kwa ajili ya waathirika, kugawa misaada ya kibinadamu na vyakula,

kutoa huduma bure kwa majeruhi, kutoa msaada wa kisaikolojia kwa waathirika, kugharamia mazishi ya watu wote waliopoteza maisha pamoja na kutoa rambirambi kwa wafiwa.

*191.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeratibu urejeshaji hali kwa wafanyabiashara waliokuwa na mikopo kupitia taasisi za kifedha walizokopa ambapo baadhi yao mikopo yao imelipwa na bima na wengine walipata nyongeza ya muda wa marejesho ya mkopo kwa kupata muda wa kipindi cha neema pamoja na kugawa pembejeo za kilimo kwa wale ambao mashamba yao yameathirika. Aidha, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa nyumba 108 kwa wakazi walioathirika na maafa na kupoteza nyumba zao na kujenga soko jipya la mbogamboga na matunda katika mji wa Katesh.

*192.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Serikali itaendelea kuimarisha usimamizi wa maafa nchini ili kuongeza ustahimilivu wa jamii dhidi ya majanga kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya uokoaji na huduma za kibinadamu ili kuongeza utayari wa kukabiliana na maafa hapa nchini. Vilevile, Serikali itaendelea kuzijengea uwezo timu na Kamati za Usimamizi wa Maafa katika ngazi za Mikoa na Wilaya, kutoa elimu kwa umma na kukiwezesha Kituo cha Taifa cha Mawasiliano na Dharura kufanya ufuatiliaji wa hali ya maafa nchini.

**Uratibu wa Masuala ya Lishe**

*193.* ***Mheshimiwa Spika,*** Maendeleo ya Taifa lolote pamoja na mambo mengine, yanahitaji uwepo wa watu wenye afya njema na lishe bora ili kuwawezesha kufanya kazi kwa bidii na tija. Kwa kutambua hilo, Serikali imeendelea kuimarisha mazingira wezeshi kwa wadau ili kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa afua za lishe, kwa kuzingatia malengo na shabaha za Mpango Jumuishi wa Pili wa Taifa wa Lishe 2021/2022 – 2025/2026. Kupitia utekelezaji wa Mpango huo, utapiamlo kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano hususani udumavu umepungua kutoka asilimia 34 mwaka 2018 hadi asilimia 30 mwaka 2022, na utapiamlo mkali kufikia chini ya asilimia tano, sawa na malengo ya Shirika la Afya ya Duniani. Aidha, hadi kufikia Februari, 2024 jumla ya shilingi bilioni 7.9 zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa afua za watoto chini ya umri wa miaka mitano.

*194.* ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania pia imeanza kufanya Utafiti wa gharama ya Utapiamlo ikiwa ni utekelezaji wa maazimio ya viongozi wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika kupitia mpango ujulikanao kama *"The Cost of Hunger in Study in Africa – COHA".* Kwa kufanya hivyo Tanzania inakuwa miongoni kwa nchi za mwanzo Barani Afrika kufanya utafiti huo muhimu ambao unalenga kuinua dhana ya umuhimu wa kukabiliana na changamoto za utapiamlo miongoni mwa jamii barani Afrika kwa kubainisha

gharama na athari zake kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Matokeo ya utafiti huu pia yatatumika kama nyenzo bora ya uhamasishaji kwa viongozi wa Serikali na watunga sera kupitia majukwaa mbalimbali ili kuchagiza hatua zaidi katika mapambano ya kutokomeza utapiamlo.

*195.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Pili wa Kitaifa wa Masuala ya Lishe wa Mwaka 2021/22 - 2025/26, kufanya tafiti mbalimbali za kisayansi kuhusu masuala ya lishe, kuratibu vikao vya majadiliano na mashirikiano na wadau wa lishe ili kufanya tathmini ya muda wa kati na kujadili utekelezaji Mpango huo pamoja na kupanga mikakati ya pamoja itakayowesha Taifa kufikia malengo yaliyowekwa.

**Mazingira**

*196.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu shughuli za utekelezaji wa hifadhi ya mazingira na kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira nchini na mabadiliko ya tabianchi kupitia usimamizi na uratibu wa utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Mikakati mbalimbali ya kitaifa pamoja na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa ya Hifadhi ya Mazingira ambayo Tanzania ni mwanachama.

*197.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi ya uhifadhi na utunzaji

wa mazingira ni pamoja na kutengwa na kuhifadhiwa kwa misitu ya jamii yenye ukubwa wa hekta 22,971 katika Halmashauri za Wilaya za Iringa, Wanging'ombe, Mbarali, Mbeya, Sumbawanga, Mpimbwe na Tanganyika ili kuhakikisha mazingira na vyanzo vya maji vinahifadhiwa.

*198.* ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi ilishiriki Mkutano wa 28 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi (COP 28) uliofanyika Tarehe 30 Novemba hadi 12 Disemba 2023, Dubai, Umoja wa Falme za Kiarabu. Ushiriki wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan katika Mkutano huo umeiwezesha nchi yetu kuendelea kuimarisha mashirikiano na Jumuiya za Kimataifa na kikanda pamoja na kuibua fursa zaidi za miradi, uwekezaji na utafiti katika sekta mbalimbali za ustawi wa jamii na ukuaji wa uchumi zenye mnasaba na masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

*199.* ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa rai kwa Wizara, Taasisi za Serikali, Asasi za kiraia na Sekta Binafsi, kuendelea kutekeleza makubaliano, maazimio na kufuatilia utekelezaji wa ahadi zilizotolewa katika mkutano huo ili kuleta manufaa ya mkutano huo wa COP28 katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

*200.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ya kukabiliana na changamoto za kuhifadhi mazingira ikiwemo athari za mabadiliko ya tabianchi. Utekelezaji huo utazingatia miradi inayoendelea na miradi mipya itakayoibuliwa ambapo itagharamiwa kupitia fedha za ndani na kutoka kwa washirika wa maendeleo na mifuko ya kimataifa ya mazingira pamoja na kuratibu utekelezaji wa makubaliano ya kikanda na kitaifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

**Uchumi wa Buluu**

*201.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kujenga mazingira wezeshi ya kutumia fursa zinazopatikana katika uchumi wa buluu kwa maslahi mapana ya Taifa. Katika mwaka 2023/2024 Serikali imeendelea na ukamilishaji wa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu pamoja na Mkakati wa Utekelezaji. Vilevile, imefufua na kuimarisha utendaji wa Shirika la Uvuvi (TAFICO) kwa kukamilisha ununuzi wa mtambo mmoja wa kuzalisha barafu na ukarabati wa miundombinu ya makao makuu ya shirika. Aidha, Serikali imekamilisha taarifa ya tathmini ya athari za mazingira na kijamii na kuanza Upembuzi Yakinifu utakaowezesha ununuzi wa meli za uvuvi katika bahari kuu.

*202.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali imelenga kukamilisha ununuzi wa meli za uvuvi katika bahari kuu, ujenzi wa kiwanda cha

kusarifu samaki Kilwa na ujenzi wa masoko ya samaki ili kuhakikisha Taifa linanufaika na rasilimali za uchumi wa buluu.

**Utawala Bora**

*203.* **Mheshimiwa Spika**, katika eneo la utawala bora Serikali imeendelea kuboresha mfumo wa utendaji wa taasisi za Haki Jinai nchini ambapo tarehe 15 Julai 2023, Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai Nchini chini ya uongozi wa Mheshimiwa Jaji Mkuu (*Mst.*) Mohamed Chande Othman iliwasilisha ripoti kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania *Mheshimiwa Dkt.* Samia *Suluhu Hassan* ikibainisha mapendekezo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha mfumo huo.

*204.* ***Mheshimiwa Spika,*** mapendekezo yaliyobainishwa na Tume ya Haki Jinai yaliridhiwa na Mheshimiwa Rais, ambaye alielekeza iundwe Kamati yenye wajumbe wa iliyokuwa Tume ya Haki Jinai na kufanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa. Hadi Machi 2024, Kamati hiyo imetekeleza kazi mbalimbali ikiwemo kuandaa rasimu ya mkakati wa utekelezaji ambao umebainisha mikakati, shabaha na afua mbalimbali za utekelezaji kwa ajili ya kuboresha taasisi za Haki Jinai nchini.

*205.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai ili kuimarisha upatikanaji wa haki nchini ambayo ni dhamira ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan. Aidha, ili kuhakikisha utekelezaji unafanyika kama ilivyokusudiwa, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele na kuziwezesha taasisi za Haki Jinai kutekeleza mapendekezo ya Tume ili kufikia malengo yanayotarajiwa.

**TEHAMA**

*206.* ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwahudumia wananchi kwa ufanisi na kuongeza tija, Serikali imeendelea kuimarisha matumizi ya Mifumo ya TEHAMA na kuhakikisha mifumo hiyo inayosomana. Hadi kufikia Machi 2024, jumla ya mifumo 130 ya Taasisi za Umma 119 imeunganishwa na inabadilishana taarifa. Hii ni katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuwa na mifumo michache na inayobadilishana taarifa. Katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuboresha, kuhuisha na kuunganisha mifumo ya TEHAMA pamoja na kuimarisha usalama wa mifumo hiyo.

## MUUNGANO

*207.* ***Mheshimiwa Spika,*** wakati tukielekea kuadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Serikali imeendelea kuchukua hatua madhubuti za kuimarisha Muungano kwa manufaa ya wananchi wa pande zote mbili ikiwa ni pamoja na kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

*208.* ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali zote mbili zina nia ya dhati na thabiti ya kuhakikisha hoja zote za Muungano zilizobaki na zitakazojitokeza zinashughulikiwa kwa ushirikiano mkubwa kwa lengo la kuulinda na kuudumisha Muungano wetu.

*209.* ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali inaendelea na maandalizi ya sherehe za miaka 60 ya Muungano ambapo uzinduzi wa sherehe hizo utafanyika Zanzibar na kilele cha maadhimisho hayo kufanyika katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, napenda kutoa wito kwa taasisi zote za Serikali na sekta binafsi kuendelea kushiriki kikamilifu katika maandalizi na maadhimisho hayo ya miaka 60 ya Muungano wetu wa kipekee na adhimu.

*210.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kutekeleza miradi na programu mbalimbali za maendeleo zinazotekelezwa pande zote mbili za Muungano kwa ajili ya kuendelea kuimarisha Muungano.

## USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA

### Mahusiano ya Kimataifa na Kikanda

*211.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mahusiano na ushirikiano na mataifa mengine duniani, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishiriki katika shughuli mbalimbali za kikanda na kimataifa ili kuimarisha utekelezaji wa diplomasia ya kiuchumi kwa lengo la kuiwezesha nchi yetu kulinda na kutetea maslahi yake kisiasa, kijamii na kiuchumi ndani na nje ya mipaka yetu.

*212.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/2024 Serikali iliratibu ushiriki wa nchi katika majukwaa mbalimbali ya kikanda na kimataifa na ziara za kikazi za kimataifa za Viongozi Wakuu ambapo Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine walitembelea nchi mbalimbali. Kutokana na ziara hizo nchi imenufaika na fursa mbalimbali za kiuchumi na kijamii kama vile masoko ya bidhaa za kilimo na mifugo zilizozalishwa hapa nchini, kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka nje, ongezeko la wafanyabiashara na wawekezaji kutoka nje, kuvutia uwekezaji wa mitaji na

teknolojia, miradi mikubwa na ya kati, upatikanaji wa misaada na kuwezesha watanzania kunufaika na ajira na ufadhili wa masomo ughaibuni.

*213.* ***Mheshimiwa Spika,*** pia katika kipindi hiki, Serikali iliratibu ziara za viongozi wakuu kutoka mataifa mengine na wawakilishi wa mashirika ya kikanda na kimataifa kutembelea nchini ikiwemo ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Andrzej Duda, Rais wa Jamhuri ya Poland, ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Klaus Iohannes, Rais wa Jamhuri ya Romania, ziara ya kikazi ya Mheshimiwa *Dkt.* Frank-Walter Steinmeier, Rais wa Jamhuri ya Shirikisho la Ujerumani, ziara ya kitaifa Mheshimiwa Joko Widodo, Rais wa Jamhuri ya Indonesia, ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Katalin Novák, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Hungary, ziara ya kitaifa ya Mheshimiwa Salvador Valdés Mesa, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Cuba na ziara ya kikazi ya Mhe. Liu Guozhong, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Watu wa China Januari, 2024. Ziara hizi ni zimesaidia kuimarisha ushirikiano baina ya nchi yetu na mataifa mengine duniani.

*214.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali bado ina nia ya dhati ya kutoa Hadhi Maalum kwa Diaspora ambao ni raia wa nchi nyingine wenye asili ya Tanzania kwa kuzingatia maombi waliyowasilisha Serikalini. Katika kutekeleza suala hili, mapitio ya Sera Mpya ya Mambo ya Nje yamejumuisha masuala ya Diaspora. Aidha, ili

kufanikisha utoaji wa Hadhi Maalum, Serikali pamoja na masuala mengine imepanga kuweka mifumo ya utambuzi na vigezo vitakavyozingatiwa.

**SERIKALI KUHAMIA DODOMA**

*215.* ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutekeleza kwa vitendo zoezi la Serikali kuhamia Dodoma ili kuhakikisha huduma za Serikali zinatolewa urahisi na ufanisi zaidi katika Makao Makuu ya nchi.

*216.* ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza hilo, katika mwaka 2023/2024, Serikali imeendelea na Awamu ya Pili ya ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi pamoja na kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya barabara za kisasa katika Mji wa Serikali Mtumba. Ujenzi wa Majengo ya Ofisi wa Awamu ya Pili katika mji huo umefikia wastani wa asilimia 75.5 ambapo tayari Ofisi na Wizara tatu zimeshamia katika majengo mapya. Ni matarajio yetu kuwa Ofisi na Wizara zilizobaki zitahamia katika majengo mapya ifikapo mwishoni mwa Juni, 2024.

*217.* ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu wezeshi katika Mji wa Serikali ikijumuisha ujenzi wa mfumo wa usambazaji umeme wa chini ya ardhi, huduma za TEHAMA na maji taka. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 27.59 zimelipwa kwa ajili ya malipo ya fidia

ya wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa kwa ajili ya kuongeza eneo litakalotumika kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Serikali.

*218.* ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/2025, Serikali itaendelea kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi wa majengo ya ofisi za wizara na taasisi na pamoja na miundombinu wezeshi katika mji huo. Vilevile, itaanza maandalizi ya ujenzi wa awamu ya tatu na mwisho ya ofisi za wizara na taasisi, eneo lililotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Serikali pamoja na uendelezaji wa miradi ya kimkakati katika makao makuu ya nchi.

## SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO

*219.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kwa kutambua umuhimu wa kukuza utamaduni, sanaa na michezo imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha sekta hizo kwa kuzingatia kuwa sekta hizo ni chachu ya kuendeleza utamaduni wa Mtanzania, utambulisho wa Taifa, chanzo kikubwa cha ajira, kuimarisha afya pamoja na kuchangia katika pato la Taifa.

*220.* ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukuza lugha ya Kiswahili Kimataifa, Serikali imeanzisha vituo vipya viwili vya kufundisha Kiswahili kwa wageni katika Balozi zetu nchini Ufaransa na Uturuki na vituo 9 katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Arusha. Jitihada hizo zimewezesha nchi yetu kuwa na jumla ya vituo 44

vya kufundisha Kiswahili kwa wageni. Mkakati uliopo ni kuwa na vituo vya kufundisha Kiswahili katika Balozi zote za Tanzania kama njia ya kubidhaisha Kiswahili Kimataifa.

*221.* ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia, imeendelea kuimarisha Mfuko wa Utamaduni na Sanaa ili kuwawezesha wasanii kuendeleza kazi zao kwa kuwapa mikopo na elimu ya ujasiriamali. Hadi kufikia Februari, 2024 mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 2.39 ilitolewa kwa miradi 113 ya Utamaduni na Sanaa ambapo miradi hiyo imewanufaisha wasanii 230,685, ambapo kati ya hao wanawake ni 131,492 sawa na asilimia 57 na wanaume ni 99,193 sawa na asilimia 43.

*222.* ***Mheshimiwa Spika,*** Napenda kumpongeza Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa na maono, kuboresha na kuhamasisha maendeleo ya michezo hapa nchini. Kufuatia juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali katika michezo sote tumeshuhudia Timu ya Taifa ya Wanaume ikifanikiwa kufuzu na kushiriki Mashindano ya AFCON ya mwaka 2023 yaliyofanyika Januari na Februari, 2024 nchini Ivory Coast pamoja na Timu ya Taifa ya Wanawake ya Mpira wa miguu **"Twiga Stars"** kufuzu kucheza mashindano ya WAFCON yanayotarajiwa kufanyika Juni, 2024 nchini Morocco.

*223.* ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, nimpongeze sana Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kutoa motisha kwa vilabu vya ndani vinavyoshiriki mashindano ya kimataifa kupitia ***Goli la Mama*** ambapo amekuwa akitoa shilingi milioni tano kwa kila goli linalofungwa katika hatua ya makundi na shilingi milioni kumi kuanzia hatua ya robo fainali. Sote tumeshuhudia *Simba Sports Club* almaarufu *Wekundu wa Msimbazi* na *Young Africans Sports Club* almaarufu *Timu ya Wananchi* wakijitwalia shilingi milioni 45 kila mmoja katika hatua ya makundi. Aidha, Tanzania imepata mafanikio makubwa kwa kuwa nchi pekee iliyoingiza timu mbili kwenye hatua ya robo fainali ya Mashindano ya Klabu Bingwa Afrika, ikiwa ni kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania. Kufanya vizuri kwa timu zetu katika mashindano hayo kumesaidia kulitangaza soka letu kimataifa. Aidha, kufuatia matokeo yao ya michezo ya awali, ningependa kuchukua fursa hii kuzitakia klabu hizo kila la heri katika michezo ya marudiano itakayochezwa tarehe 05 Aprili, 2024.

## HITIMISHO

*224.* ***Mheshimiwa Spika,*** nikihitimisha hotuba yangu, ningependa kutoa rai kwa watanzania wote kuendelea kuliombea Taifa hususan tunapoanza maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu pamoja na kuunga mkono juhudi

za Serikali za kuwaletea maendeleo katika Sekta zote. Aidha, Ofisi ya Waziri Mkuu itaendelea *kuratibu* na kufuatilia shughuli mbalimbali za Serikali ili kuhakikisha malengo tuliyojiwekea katika Dira ya Taifa ambayo utekelezaji wake unafikia ukomo mwaka 2025 yanafikiwa.

*225.* ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kueleza kwa muhtasari baadhi ya shughuli ambazo Serikali imetekeleza kwa kipindi kilichopita na mwelekeo wa kazi zitakazofanyika kwa mwaka 2024/2025, ninapenda kusisitiza mambo muhimu yafuatayo:

**Mosi:** Kuendelea na maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo kwa kuhakikisha wananchi na viongozi wanapata muda wa kutosha kujadili na kutoa maoni pamoja na kuzingatia maoni hayo katika rasimu ya Dira;

**Pili:** Kuendelea kuimarisha jitihada za upatikanaji wa umeme wa uhakika ikiwa ni pamoja na kuongeza uwekezaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati kwa wakati katika maeneo ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa nishati ya umeme ili kuhakikisha nchi inakuwa na huduma za uhakika na zitakazovutia uwekezaji;

**Tatu:** Kuimarisha juhudi za kuongeza uzalishaji wa sukari nchini pamoja na kuvutia uwekezaji katika eneo hilo ili kuipatia ufumbuzi wa kudumu changamoto ya upatikanaji wa sukari nchini;

**Nne:** Viongozi wa dini na wananchi kwa ujumla kuliombea Taifa wakati linaingia kwenye kipindi cha maandalizi ya uchaguzi ili kuwa na amani. Aidha, natoa rai kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika hatua za maandalizi na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024 ili kutumia haki yao ya kikatiba. Vilevile, kuanza vyema maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025;

**Tano:** Kuimarisha juhudi za ukusanyaji mapato ili kuongeza uwezo wa Taifa kujitegemea, pamoja na kubana matumizi katika maeneo yasiyokuwa na tija katika utoaji wa huduma kwa wananchi;

**Sita:** Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi za Utafiti, Taasisi za Elimu, Taasisi Binafsi na Wadau kutumia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 wakati wa maandalizi ya miradi, programu na mipango mbalimbali; na kuhakikisha taarifa ya anwani za makazi zinakuwa sehemu ya taarifa ya

msingi wakati wa kutoa na kupokea huduma.

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA OFISI YA WAZIRI MKUU NA OFISI YA BUNGE KWA MWAKA 2024/2025

*226.* ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2024/2025, Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 350,988,412,000,** kati ya fedha hizo, **shilingi 146,393,990,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 204,594,422,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

*227.* ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **shilingi 181,805,233,000** kwa ajili ya Mfuko wa Bunge. Kati ya fedha hizo, **shilingi 172,124,423,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 9,680,810,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

*228.* ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.